SUPA JACKPOT
TZS. 1,142,132,257
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

WATETEZI HAKI:
**Simba** iombe radhi kwa kudhalilisha wenye ualbino
UKURASA 4


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Kasoro kimfumo zinazomweka hatarini mwandishi wa habari anapokuwa kazini
Kikundi Daraja Salama kilivyofika kuchangia damu, daktari akiwazawadia somo
Operesheni ya kuhifadhi misitu kijijini inavyopatia faida zahanati iliyotima
Ushuhuda wa vita vya Dk. Samia kutanua ulingo wa mbolea nchini
• Mageuzi ya viwanda hadi kwenye udongo shambani
UKURASA 11

Nipashe
Alhamisi Agosti 10, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581398
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

SAKATA LA BANDARI

# JK na Kinana watishia kushtaki kortini

UKURASA 2


Kinana Kikwete

UKURASA WA 3

**TANZANIA, UAE ZATIA SAINI MKATABA MKOPO USAMBAZAJI UMEME KAGERA**

TANZANIA na Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi wa Umoja wa Falme za Kiarabu, zimetiliana saini mkataba...



UKURASA WA 4

MARUFUKU USHOGA

**BENKI YA DUNIA YASITISHA MIKOPO MIPYA UGANDA**

BENKI ya Dunia imesema itasitisha utoaji mikopo mipya kwa serikali ya Uganda baada ya kuafiki...

UKURASA WA 19

**UGUNDUZI MAFUTA YA SENENE KUTIBU MOYO**

TEKNOLOJIA za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ikiwamo kumwongezea thamani senene kwa...

## Waziri: Ukilipishwa tiba malaria toa taarifa tuchukue hatua

UKURASA 2



## Mbowe alalama Kanda ya Ziwa hawanufaiki na utajiri wa madini

UKURASA 3

MICHEZO **YANGA YATINGA FAINALI KIBABE** UK.24

KATUNI UK.6

# JK, Kinana watishia kuishtaki MwanaHalisi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana, wameonyesha nia ya kufungua kesi dhidi ya kampuni ya Hali Halisi Publishers Ltd, ambao ni wachapishaji wa gazeti la MwanaHalisi.

Viongozi hao wametishia kuchukua hatua hiyo kwa kile walichodai tuhuma zilizoandikwa dhidi yao kuhusu sakata la Bandari kuwa ni za uongo, zimewatweza, kuwashushia hadhi na kashfa zenye lengo la kuwafedhehesha.

Kwa mujibu wa kusudio hilo la Agosti 7, mwaka huu, kutoka kwa Kampuni ya Uwakili ya Eric S. Ng'maryo ya mjini Moshi, iliyotiwa saini na Wakili Patricia Eric ambaye ni Mbia Mtendaji na Eric Ng'maryo, wateja wao wamewaagiza kufikisha kusudio hilo kwa kuwataka MwanaHalisi baada ya kupata barua kuchapisha kwenye ukurasa wa kwanza kwa vichwa vya habari, ambavyo vitafanana kadiri iwezekanavyo kwa ukubwa wa herufi na mtindo wa uchapaji uliotumika katika kuchapisha habari za kashfa dhidi yao.

Pia wameelekeza habari hiyo iende na picha za wateja wao zilizojitokeza wazi, makala yenye tamko mwafaka la kufuta kashfa iliyo katika gazeti na kuwaomba radhi wateja kwa kashfa hiyo kwa kujumuisha udhuru, stahili au shaka. Kabla ya kuchapisha habari hiyo na kuomba radhi, wamemtaka Mhariri wa MwanaHalisi apeleke kwa mawakili hao rasimu ya tamko hilo kwa barua pepe kwa ajili ya kuhaririwa.

"Kama tamko la kufuta kashfa na kuomba radhi halitakubaliwa kabla ya kuchapishwa, basi tamko hilo linaweza kushindwa kukidhi dai la barua hii. Pamoja na tamko la kufuta kashfa na kuomba radhi na kwa wakati huo huo ambao tamko litatolewa, Mhariri wa MwanaHalisi atatakiwa kutoa kiapo cha kisheria akitamka kwamba yeye (Saeed Kubenea/mhariri) na gazeti analolihariri, wanaahidi kuacha kuwakashfu au kutoa namna yoyote ya matusi au maneno ya uongo, kero au uchafuzi dhidi ya wateja wetu wawili," alisema.

"Iwapo Bodi ya Wakurugenzi ya HaliHalisi Limited, uongozi wa kampuni na mhariri wa gazeti wataafiki kutekeleza yale yanayodaiwa katika barua hii, na iwapo watafanya hivyo bila ajizi wala kuzuizi katika kipindi cha siku 14 kutoka tarehe ya kufikishwa barua hii kwa MwanaHalisi kwa njia ya barua pepe. Basi wateja wetu wataacha kuchukua hatua za kisheria au kiutawala dhidi ya wale wote waliohusika katika kashfa inayolalamikiwa dhidi ya gazeti," aliongeza.

Akizungumza na Nipashe kwa simu, Wakili Patricia alithibitisha kusudio hilo kutolewa na kampuni hiyo ikiwa na dai la kufuta kashfa na kuomba radhi pamoja na ahadi ya kuacha kukashifu.

"Atalipata kusudio letu muda wowote kuanzia sasa (saa 6:12 mchana alivyoongea na Nipashe) na kama hatatimiza yale yaliyotakiwa basi tutaendelea na hatua inayofuata kwa kwenda mahakamani," alisisitiza.

Kwa mujibu wa kusudio hilo, viongozi hao wanadai kutendewa hayo kupitia habari iliyochapishwa Julai 20 hadi 26, mwaka huu, katika ukurasa wa mbele ikiwa na kichwa cha habari elekezi cha maandishi ya wino mwekundu kisemacho: "Sakata la Bandari" chini yake kukiwa na bango la kichwa cha habari kikuu chenye wino uliokolea kikinadi "JK, Kinana, Karamagi watajwa".

"Hilo bango la kichwa cha habari limepewa uzito wa pekee maana maandishi yake ni makubwa kuliko hata maandishi ya jina la gazeti. Si hayo tu bali pia juu kulia mwa gazeti ipo picha ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete yenye ukubwa sawa na thumuni (moja ya nane) ya ukurasa wa mbele wa gazeti na maelezo ya chini ya picha yanasema Jakaya Kikwete.

"Picha ya ndugu Abdulrahman Kinana nayo iko katika ukurasa wa mbele akiwa amevaa shati la rangi ya kijani na manjano ambazo ni rangi za sare za CCM. Chini ya picha ya Kikwete katika ukurasa wa kwanza kipo kichocheo cha habari kusemacho "serikali yajitetea kutumia fedha kulainisha wananchi".

Kusudio hilo lilieleza kuwa katika ukurasa wa kwanza wa gazeti, aya elekezi inamtambulisha Kikwete kwamba ni Rais Mstaafu na Kinana ni Makamu Mwenyekiti wa CCM (Bara) yenye ukubwa wa sentimita 24 kati ya 30 za urefu wa maandishi ya ukurasa wa mbele wa gazeti.

"Katika ukurasa huo wa mbele kimo kiashiria cha rangi nyekundu kionyeshacho kwamba makala ya ukurasa wa kwanza inaendelea ukurasa wa pili, ukurasa wa pili umefunikwa na makala iliyoanza ukurasa wa kwanza na haijaingiliwa na kitu kingine chochote mbali na picha za wale wanoongelewa katika makala hiyo, zikiwamo picha zilizo katika eneo la mduara zikiwaonyesha Kinana na Kikwete.

"Makala inamwagikia ukurasa wa tatu wa gazeti ambapo msomaji anakumbushwa kwa kichwa cha habari "JK, Kinana, Karamagi watajwa. Kifupi JK kimekuwa kikitumika mara nyingi kumtambulisha Mheshimiwa Jakaya Kikwete," lilisema kusudio hilo.

Kusudio hilo lilieleza kuwa wakati gazeti linachapisha, mjadala wa kitaifa uliopo nchini kuhusu Bandari umetambuliwa na gazeti katika maoni ya mhariri na pia katika makala mbalimbali zilizotanda kwenye ukurasa wa nane kati ya kurasa zote 20 za gazeti na kwamba mjadala huo umesisitizwa na gazeti kuwa ni muhimu na mtata kwa kuelezwa kuwa ni "Sakata la Bandari".

Aidha, lilibainisha kuwa katika kurasa zilizozungumzia mjadala wa Bandari, waandishi mbalimbali wametoa maoni yao kuhusu suala hili na kwamba iliwapasa kutaja kwamba umuhimu wa mada ya bandari umethibitishwa katika ukurasa wa 10 na 11 na katika kurasa hizo mbili kwa pamoja zinachambua suala mojawapo kati ya masuala kadhaa kuhusu bandari.

"Kashfa katika gazeti inayowadhalilisha wateja wetu imewagusa kwa kutamka moja kwa moja na kwa kuweka sambamba vichwa vya habari, maelezo ya picha na picha zenyewe katika nia ovu ya kuyakinisha kashfa iliyotolewa dhidi ya wateja wetu. Chanzo cha kashfa katika gazeti dhidi ya wateja wetu inasemwa na gazeti kwamba ipo katika 'kipeperushi' kilichoonekana mitandaoni... kwa mantiki hiyo, gazeti linakubali kwamba hayo yaliyomo katika gazeti linachokita kipeperushi ni kashfa dhidi ya wateja wetu.

"Mbali na kukubali na kushuhudia kashfa hiyo tajwa, gazeti linashuhudia pia kwamba hicho 'kipeperushi' ni chanzo cha habari chenye uzushi mtupu... kiini cha kashfa iliyopo katika gazeti dhidi ya wateja ni kwamba wateja hao wawili wanaopinga maendeleo ya Bandari za Tanzania, hususani maendeleo ya Bandari hizo kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa kati DP World ya Dubai na serikali ya Tanzania.

"Hiyo kashfa haiishii hapo bali inaongeza kutamka uongo mwingine kwamba wateja wetu (wakishirikiana na watu wengine) wanachochea wale wanaopinga maendelezo ya Bandari kwa kuwalipa fedha watu ambao hawajatajwa ili watu hao wapinge au waendelee kupinga maendelezo ya Bandari. Baadhi ya tuhuma hizo ni za uongo na za kashfa zipo katika ukurasa wa pili safu ya gazeti," lilisema kusudio hilo.

Aidha lilifafanua kuwa: "Bila kueleza kwa kirefu sifa njema na utumishi wa siasa uliotukuka wa wateja wetu wawili, tungependa kusema kwa kifupi kwamba Ndugu Kinana wa CCM ndio chama cha siasa kilichounda serikali iliyoko madarakani na mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Kikwete ni Mwenyekiti Mstaafu wa CCM na Rais Mstaafu.

"Mwana Halisi lina wasomaji maelfu na idadi hiyo inaweza kufikia mamilioni ya wasomaji Tanzania na duniani wanakolipata gazeti. Upeo wa kuumizwa na kuathiriwa na kashafa iliyochapishwa katika gazeti dhidi ya wateja wetu ni mkubwa kwa athari, upana na wingi wa wasomaji. Hiyo ni athari ya kudumu kwa kuhesabu miaka ya uwepo wa athari hiyo katika macho ya wasomaji.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DIVISHENI YA KAZI**
**DAR ES SALAAM**

**DENI TUZO NO. 234 YA 2023**

**BAINA YA**

**ARLENE GOMES.....................................MUOMBAJI**

**NA**

**MINING AGRICULTURE & CONSTRUCTION SERVICE..........................MJIBU MAOMBI**

**Kwa:**
**MINING AGRICULTURE & CONSTRUCTION SERVICE,**
**DAR ES SALAAM**

Mnajullishwa kwamba shauri la maombi ya deni tuzo tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es salaam tarehe **16/8/2023** saa tatu asubuhi **(3.00).** Mbele ya mheshimiwa **S.R.DING'OHI-NAIBU MSAJILI MFAWIDHI** Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hamtahudhuria nyinyi au wawakilishi wenu wanaotambulika kisheria basi maombi hayo yatasikilizwa bila uwepo wenu.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe **18/7/2023**



**NAIBU MSAJILI MFAWIDHI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DIVISHENI YA KAZI**

17546002


# Waziri: Ukilipishwa tiba malaria toa taarifa ili tuchukue hatua

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameagiza wananchi kutoa taarifa pindi wanapotozwa fedha za matibabu ya malaria katika vituo vya afya ili wahusika wachukuliwe hatua.

Pia amewataka wataalam waache kitu alichokiita 'uhuni' katika suala hilo kwa sababu dawa, sindano na kipimo cha haraka cha ugonjwa huo kinatakiwa kutolewa bure.

Ummy alitoa kauli hiyo jana Temeke wakati wa ziara yake ya kutatua changamoto ya ufinyu wa maeneo unaozikabili hospitali na vituo vya afya mkoani Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo pia alitembelea Hospitali ya Mbagala Rangi Tatu na kukagua mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo itakayokuwa na ghorofa sita na itagharimu Sh. bilioni 10.8 Waziri huyo alisema wakisikia hakuna dawa, wananchi wasimlaumu Rais Samia Suluhu Hassan bali wamlaumu yeye, mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri ambao ndio watendaji.

"Nimefurahi mmefanya ziara shirikishi kwenye vituo. Dawa za anti-malaria (za kutibu na kupambana na malaria) hazitakiwi kukosekana kwa sababu ni bure na vipimo vya malaria ni bure. Hili ninataka kulisisitiza, wataalam wetu waache uhuni. Dawa za malaria (ARUO zinapaswa kutolewa bure bila malipo yoyote.

"Sindano ya malaria kali 'Artesunate' inapaswa kutolewa bure. kipimo cha haraka cha Malaria RDT kinapaswa kupimwa bure ," alisema.

Katika ziara hiyo, Waziri Ummy alisema Rais Samia ameahidi kutoa Sh. bilioni mbili katika ujenzi wa jengo la ghorofa sita la Hospitali ya Mbagala Rangi Tatu ambalo litagharimu Sh. bilioni 10.8 ili kupunguza msongamano wa wagonjwa hospitalini hapo .

"Nilifanya ziara hapa mwaka 2020 na mwaka 2021 nikapokea kero ya msongamano wa wagonjwa katika hospitali hii na kuipeleka kwa Rais Samia na ametoa Sh. bilioni mbili ili kukamilisha ujenzi huu", alisema Waziri Ummy.

Alisema Rais Samia yuko tayari kutoa fedha za huduma, kwani idadi ya watu imekua ikiongezeka ndani ya Wilaya ya Temeke na kwa sasa kila mwezi anatoa fedha za dawa.

HABARI KITAIFA



Balozi wa Finland nchini Tanzania, Theresa Zitting (kulia) na Mkurugenzi wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN), Elizabeth Riziki (katikati) wakisaini mkataba wa utekelezaji mradi wa kuboresha utendaji wa vyombo vya habari na mabadiliko ya sheria kwa kushirikiana na taasisi ya Protection Africa International (PAI). (kushoto) ni Mwenyekiti wa MISA TAN, Salome Kitomari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania, UAE zatia saini mkataba mkopo usambazaji umeme Kagera

**Na Benny Mwaipaja,**
ABU DHABI

TANZANIA na Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi wa Umoja wa Falme za Kiarabu, zimetiliana saini mkataba wa mkopo nafuu wa dola za Marekani milioni 30 (Sh. bilioni 70) kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovolti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka.

Sambamba na usafirishaji huo, mkopo huo pia ni kwa ajili ya upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kyaka mkoani Kagera.

Mkataba huo ulitiwa saini jana makao makuu ya mfuko huo, mjini Abu Dhabi na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kwa niaba ya serikali Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi (ADFD), Mohammed Saif Al Suwaidi.

Dk. Nchemba alisema mradi huo utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme umbali wa kilometa 167 kutoka Benaco hadi Kyaka na kwa mujibu wa Wizara ya Nishati, hadi mradi huo utakapokamilika unatarajia kugharimu dola za Marekani milioni 119.4.

"Mkopo huu tuliotia saini utachangia nguvu zilizotolewa na mifuko mingine ukiwamo OPEC Fund for International Development uliotoa dola za Marekani milioni 60, Mfuko wa Maendeleo wa Saudia uliotoa dola za Marekani milioni 13 na serikali ya Tanzania iliyochangia dola za Marekani milioni 2.4," alisema.

Kukamilika kwa mradi wa umeme wa Benaco-Kyaka, kutaimarisha hali ya upatikanaji umeme katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ambayo imekuwa na changamoto ya umeme pungufu na usio wa uhakika. Hatua hiyo pia itaufanya mkoa wa Kagera kuanza kutumia umeme wa gridi ya taifa badala ya ule wa kutoka Uganda.

Dk. Nchemba aliipongeza ADFD kwa kuunga mkono jitihada za serikali za kuwaletea wananchi maendeleo kupitia miradi ya nishati ambao utakuza uchumi na ajira kwa wakazi wa maeneo ambayo umeme utapitishwa.

"Mpaka sasa Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi umewekeza Tanzania Dola za Marekani milioni 96.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii na umekuwa mdau mkubwa wa maendeleo ya nchi kwa muda mrefu," aliongeza Dk. Nchemba.

Al Suwaidi alisema mfuko wake utaendelea kufadhili miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Tanzania ili nchi ifikie malengo yake ya kuwaletea wananchi maendeleo kuoitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

"Mradi huu wa kimkati wa kusambaza nishati ya umeme kwa wananchi ni hatua muhimu kwa ajili ya kufikia malengo na matamanio ya wananchi ya kujiletea maendeleo lakini ni kielelezo pia cha ushirikiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na Umoja wa Nchi za falme za Kiarabu ambao wameweka mipango ya kuendelea kushirikiana na Tanzania kwa kuwa ni mdau mkuu wa maendeleo," alisema Al Suwaidi

Alisema mfuko huo utaendelea kuangalia fursa zingine za ushirikiano katika nyanja mbalimbali za kiuchumi zinazopatikana Tanzania ikiwemo sekta ya utalii, kilimo, ujenzi wa makazi ya kisasa kwa ajili ya watumishi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, miundombinu ya barabara, kilimo pamoja na nishati.

Miongoni mwa miradi ambayo mfuko huo umetoa fedha kwa Tanzania ni pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Wete-Pemba, barabara ya Kidawe hadi Uvinza (km 77), ujenzi wa kiwanda cha Sukari Kagera na mradi wa maji vijijini Zanzibar ambayo imekamilika na kwa sasa unafadhili ujenzi wa barabara ya Uvinza-Ilunde hadi Malagarasi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 15.

# Freeman Mbowe: Kanda ya Ziwa haijanufaika kuwapo dhahabu

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema kuwapo dhahabu Kanda ya Ziwa haujawanufaisha wakazi wa eneo hilo.

Mbowe alitoa kauli hiyo jana wakati akihutubia wananchi wa Nyarugusu mkoani Geita ikiwa ni mwendelezo wa mikutano ya hadhara ya viongozi wa chama hicho wanayoifanya nchi nzima, iliyopewa jina la 'operesheni +225 Katiba mpya'.

Alisema kwa namna Kanda ya Ziwa ilivyo na rasilimali nyingi ilipaswa iwe juu kwenye uchumi, lakini wananchi wake hawajanufaika vizuri na uwapo wa rasilimali hizo.

Alisema hilo ni tatizo linalosababishwa na kukosekana kwa mifumo mizuri ya kutumia rasilimali hizo zinufaishe wananchi.

"Dhahabu yetu Kanda ya Ziwa haijaonyesha kuleta neema kwa wananchi wa kanda hii, dhahabu imesambaa kuanzia Mara, Geita, Kagera, Tabora. Ni ukanda wote umejaa dhahabu, lakini pamoja na hayo yote bado kuna umaskini," alisema Mbowe.

"Mipango iliyopo haijawapelekea wananchi kunufaika na rasilimali zao. Ukanda huu unaongoza kwa rasilimali ardhi, mifugo, ziwa, pamba lakini bado kuna shida nyingi kutokana na kukosekana kwa mipango mizuri ya kuitumia iwanufaishe," alisema Mbowe.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Zanzibar, Salum Mwalimu, alisema shida inayochangia wananchi katika kanda hiyo kutonufaika na rasilimali zilizopo ni sera mbaya za usimamizi wa uchimbaji mdogo wa dhahabu.

"Mali kidogo walizonazo wananchi wa kanda hiyo wanazowekeza kwenye uchimbaji mdogo kama njia ya kuondokana na umaskini wa kipato, lakini bado haisaidii kwa sababu ya sera mbaya zilizopo za uchimbaji huo mdogo," alisema Mwalimu.

Aliwataka wananchi wa Nyarugusu kukichagua chama hicho katika uchaguzi mkuu ujao mwaka 2025 na wa serikali za mitaa mwaka ujao.

"Ili tuweze kusimamia sera za uchimbaji madini mdogo, tuchagueni katika chaguzi zijazo na nina waahidi ndani ya mwaka mmoja hamtaamini mabadiliko yatakayotokea," alisema Mwalimu.

"Kuendelea kupiga kelele na kulia haitusaidii kama bado hatuko tayari kuchukua maamuzi magumu. Sera ya uchimbaji madini ya CHADEMA ni bora, tumeiandika na tumeieleza, haiwezekani mchimbaji mdogo akashindwa kunufaika kwenye ardhi ya nchi yake kwa sababu anatafuta kipato cha kuiendeleza familia yake.


IOGT·NTO·MOVEMENT

**Publication of Bi-Annual Income and Expenditure**

**IOGT-NTO Movement** is a Swedish organization, registered in Tanzania as an International NGO, addressing the alcohol harm in Tanzania, Burundi, Kenya, Rwanda, and Uganda. IOGT-NTO Movement works through local partner organizations to fulfil its goal to create strong communities where people are empowered, rights are protected and harm from alcohol and other drugs is minimized.

**Our Vision**: A democratic world characterized by solidarity and equality where alcohol and other drugs do not impede peoples' welfare, freedom and security.

**Our Mission:** To strengthen relevant actors in their work for reduced use of alcohol and other drugs in developing countries and thus contribute to democratic development, strengthen rights and reduced poverty.

| Bi-Annual Income and Expenditure Report for the Period of January to June 2023. | |
|---|---|
| **Income:** | |
| Receipt from Donors | 217,561,916 |
| **Expenditure:** | |
| Human Resource | 82,831,847 |
| Office Administration and Communication | 31,533,601 |
| Capacity Development and Networking | 0.00 |
| Quality and Compliance Monitoring | 9,013,401 |
| Planning Meetings | 1,911,918 |
| **Total Expenditure** | **125,290,767** |

IOGT NTO Movement - East Africa Office
Plot No. 43, Uporoto Street Box 7522, Dar Es Salaam Tanzania
eaoffice@iogtntomovement.se
www.iogtntororelsen.se/

217544802

WATETEZI HAKI ZA BINADAMU:

# Uongozi wa Klabu ya Simba uombe radhi

**Na Sabato Kasika**

TAMASHA la Siku ya Simba limepata doa tena. Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) wameutaka uongozi wa Klabu ya Simba kuomba radhi, kwa madai ya kudhalilisha watu wenye ulemavu huo.

Katika ofisi za LHRC jana, Mwenyekiti wa TAS, Godson Molell, akisoma tamko la kulaani matukio aliyoyaita ya udhalilishaji utu wa watu wenye ualbino, alisema klabu hiyo ilitumia albino kama mtu aliyekuwa katika hali ya nusu utupu na aliyevaa nepi jukwaani mbele ya umma kwenye Uwanja wa Mkapa.

Mollel alifafanua kwa waandishi wa habari kuwa Siku ya Simba Agosti 6, mwaka huu, kitendo hicho kilifanywa na kimesababisha kuibuka mijadala mingi katika jamii, ikiwamo mitandao ya kijamii, hali ambayo kwa tafsiri yao inayoonesha dhihaka kwa watu wenye ualbino.

"Tunawataka Simba waombe radhi kwa tukio hilo la kumtumia mtu mwenye ualbino kudhalilisha utu wa watu wenye ulemavu huo," alisema Molell.

Alisema hilo ni tukio la pili kufanywa na klabu hiyo, likitanguliwa na la mwaka jana ambalo msanii Tunda Man alitumia jeneza na kumfanya mtu mwenye ualbino aonekane msukule.

"Vitendo hivi vinatweza utu wa watu wenye ualbino. Kwa mujibu wa Ibara ya 12(2) ya Katiba ya Tanzania ya Mwaka 1977, kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake," alisema.

Alisema utani wa timu za Simba na Yanga, hauhalalishi vitendo vya kutweza utu wa mtu, iwe kwa kukusudia au bahati mbaya.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alitoa wito kwa taasisi zote zenye ushawishi kwa jamii kama timu za mpira, kuepuka vitendo hivyo, badala yake zijikite katika kuhamasisha heshima kwa utu wa watu wenye ualbino na wengine wenye ulemavu nchini.

"Tunatoa wito kwa jamii wakiwamo wenye ualbino wenyewe kutokuchukulia vitendo vya aina hii kwa wepesi, bali wavikemee vikali, kwani albino ni binadamu kama wengine wenye haki ya kutodhalilishwa utu wao," alisema Dk. Anna.

Alisema LHRC inawataka watu wenye ualbino kutokubali kutumiwa hasa kwenye mambo yanayotweza utu wao.

"Tunataka uongozi wa Simba uombe radhi kwa watu wenye ualbino na umma wa Watanzania, kwa vitendo hivi vya kutweza utu wa watu wenye ualbino, na tunaiomba serikali na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) wasimamie jambo hili," alisema.

Alifafanua kuwa Ibara ya 8 ya Mkataba wa Kimataifa wa Watu Wenye Ulemavu, inasisitiza kutolewa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya ulemavu.

"Tunaiomba serikali kutilia mkazo zaidi kukomesha masuala ya ubaguzi, udhalilishaji, unyanyasaji, mawazo mgando na vitendo vyote vinavyotweza utu wa watu wenye ulemavu, wakiwamo wenye ualbino.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, baada ya tamko hilo la watetezi wa haki za binadamu, alisema wataomba radhi, lakini sasa wamejikita katika maandalizi ya mechi yao ya kesho dhidi ya Singida FG.



Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), Godson Molell (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari, Kijitonyama Dar es Salaam jana, alipotoa tamko la kulaani timu ya Simba, kwa madai ya kudhalilisha mtu mwenye ulemavu huo na kuitaka iombe radhi. Wengine ni mratibu wa miradi wa chama hicho, Saleh Mkami, Katibu Mkuu, Baatha Mtoteye na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga. **PICHA SABATO KASIKA**

# Benki ya Dunia yasitisha mikopo mipya Uganda

**KAMPALA, Uganda**

BENKI ya Dunia imesema itasitisha utoaji mikopo mipya kwa serikali ya Uganda baada ya kuafiki kuwa sheria ya nchi hiyo dhidi ya jamii ya watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja inakinzana na maadili ya benki hiyo.

Taarifa iliyotolewa jana na benki hiyo ilibainisha kuwa hakuna ufadhili mpya wa umma utakaotolewa kwa Uganda hadi hatua za ziada na za ufanisi zitakapochukuliwa na kuongeza kuwa hatua hizo sasa zinajadiliwa na mamlaka za Kampala (Uganda).

Inaelezwa kuwa hadi mwishoni mwa mwaka 2022, Benki ya Dunia ilitoa dola bilioni 5.4 kufadhili miradi ya maendeleo Uganda ikiwa ni pamoja na miradi mingi ya afya na elimu ambayo inaweza kuathiriwa na hatua hiyo mpya.

Ujumbe wa Benki ya Dunia ulifika Uganda baada ya kuanzishwa kwa sheria inayotoa hadi hukumu ya kifo kwa kile kinachotajwa kuwa ushoga uliokithiri, kosa linalojumuisha kusambaza Virusi vya Ukimwi (VVU) kupitia ngono ya mashoga ambayo imekuwa ikikosolewa na mataifa kadhaa pamoja na Umoja wa Mataifa (UN).

Wajumbe hao waliamua kwamba kunahitajika hatua za ziada kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa kuzingatia kanuni za kijamii na kimazingira za taasisi hiyo.

Rais mpya wa benki hiyo, Ajay Banga, ambaye amekuwa anakabiliwa na shinikizo la kutoa msimamo wake juu ya sheria hiyo, alisema sheria ya kupinga ushoga ya Uganda kimsingi inakinzana na maadili ya Benki ya Dunia na anaamini maono ya kutokomeza umaskini ulimwenguni yanaweza kufanikiwa ikiwa tu yatawajumuisha watu wote bila kujali rangi yao au jinsia.

Banga alisema bado wana nia ya kuendelea kuwasaidia Waganda wote kuepuka umaskini, kupata huduma muhimu na kuboresha maisha yao lakini bila kumtenga yeyote.

Juni 15 mwaka huu, jumla ya vikundi 170 vya kiraia vilimtaka Banga kuchukua hatua mahususi na kwa wakati ili kujibu sheria ya Uganda dhidi ya mashoga ikiwa ni pamoja na kusitisha mikopo ya baadaye kwa taifa hilo.

Lakini, mfuko wa ufadhili wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kimataifa kwa Uganda utaendelea kutoa fedha kwa nchi hiyo bila kujali hatua ya kusitisha mikopo mipya.

Vilevile, benki hiyo ilieleza kuwa miradi ya sekta binafsi inayoungwa mkono na Shirika la Kimataifa la Fedha na Wakala wa Dhamana ya Uwekezaji wa Kimataifa (MIGA) itaendelea lakini kwa kuchujwa.

# Jamhuri kuzuia dhamana kesi kukutwa na kobe 116

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Mashtaka katika kesi ya kukutwa na kobe 116 inayomkabili raia wa Ukraine, Olga Kryshtopa (32) na watanzania wanane wakiwamo maofisa wa polisi, umekusudia kuwasilisha kiapo cha kupinga dhamana ya raia huyo.

Wakili wa Serikali, Elizabeth Mkude, alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Rhoda Ngimilanga wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati shauri hilo lilipoitwa kwa ajili ya kutajwa.

Wakili huyo alidai kuwa Kryshtopa ana wakili wake ambaye jana hakuwapo mahakamani, hivyo aliiomba mahakama ipange tarehe nyingine.

"Upande wa Mashtaka bado tuna nia ya kuwasilisha kiapo cha kupinga dhamana ya mshtakiwa Kryshtopa na tunaomba wakili wake akiwapo ndiyo tuwasilishe kiapo hicho," alidai Mkude.

Hakimu Ngimilanga aliahirisha kesi hiyo hadi Agosti 23 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

Washtakiwa wengine ni Josephat Moyo (52), Deogratius Lugeng'a (40), MT88046 SGT Cosmas Ndomba (39), Hamza Abdallah (32), MT118102 Kasimu Abdallah, Stephan Chedego na Mwaluko Ngomole.

Washtakiwa wawili Olga na Deogratius walirudishwa rumande na wengine saba wakiwa nje kwa dhamana wakati upelelezi wa kesi hiyo unaendelea.

Inadaiwa kuwa kati ya Januari hadi Julai 22, 2023, katika maeneo tofauti ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa wote kwa nia ovu waliongoza genge la uhalifu kwa kununua na kuuza kinyume cha utaratibu nyara za serikali ambazo ni kobe 116 wenye thamani Sh. 189,359,400, mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika shtaka la pili, inadaiwa kuwa katika tarehe tofauti Januari hadi Julai 2022, maeneo tofauti ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa wote walijihusisha na nyara za serikali bila kufuata utaratibu wa maliasili.

Katika shtaka la tatu, inadaiwa kuwa washitakiwa wote Julai 3, 2022, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), jijini Dar es Salaam, walikutwa wanamiliki kobe 116, ambao ni nyara za serikali.

# MATANGAZO

FSSP
Field Support Services Project | Tanzania

## CONSULTANCY POSITION FOR LOCAL PROJECT MONITOR FOR THREE ADOLESCENT SEXUAL AND REPRODUCTIVE HEALTH AND RIGHTS PROJECTS IN TANZANIA

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC), on behalf of our client, invites eligible candidates to express their interest to provide individual consultancy services as Local Project Monitor for Three Adolescent Sexual and Reproductive Health and Rights Projects in Tanzania through a direct support from the Canadian Department of Foreign Affairs, Trade and Development (DFATD).

The candidate will have responsibility to provide project decision-makers and other stakeholders with regular, reliable information and advice on the projects' progress, help partners make corrective adjustments as needed and, ultimately, achieve better development results. An integral part of this assignment is to provide a platform for communication and sharing of lessons learned and best practices to ultimately improve health programming in Tanzania.

**The ideal Project Monitor will possess the following key qualifications:**

- A Bachelor's degree from a recognized university.
- A minimum of twelve months of experience within the last five (5) years in providing monitoring and evaluation support at the time of the RFP closing. (12 months of experience is equivalent to 220 days.)
- Professional experience providing administrative and organizational capacity support (preferably to health stakeholders).
- Professional experience in coordinating, liaising and sharing information with Government, development partner, civil society and/or private sector stakeholders (health stakeholders preferred).
- Professional experience in applying results-based management approaches in the design, planning, monitoring and evaluation of development projects or programs (for health projects preferred).

In addition to the key qualifications above, the incumbent is also expected to demonstrate the following skills and competencies:

- Advanced professional proficiency in reading, spoken and written English – level 4+ as explained in **http://www.international.gc.ca/ifait-iaeci/test_levels-niveaux.aspx?lang=eng** and the ability to work in Kiswahili will be a significant asset.
- Knowledge of the Health Sector policy priorities and processes in Tanzania, including planning, management and budgeting of public sector resources. Experience with maternal and newborn, child health (MNCH), Sexual Reproductive Health and Rights (SRHR), health systems strengthening (HSS), Sexual Gender Based Violence (SGBV) as well as work in community-level initiatives is an asset.

Interested individual candidates should obtain a detailed description of these services by sending a request email to **procurement@fssptz.org.** Requests for further information will be received up to three (3) working days prior to the submission deadline. Any request received later than that may not be responded to.

Interested candidates should send their Expressions of Interest (EoIs) ONLY electronically to **procurement@fssptz.org** not later than **20 August 2023 at 23:59 hours.** Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation, irrespective of the circumstances.

**FSSP Manager**

**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

## TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA WADAU WA TASNIA YA KOROSHO MWAKA 2023

Bodi ya Korosho Tanzania inapenda kuwaarifu Wadau wote wa Tasnia ya korosho nchini kuwa mkutano mkuu wa Wadau wa tasnia ya korosho utafanyika tarehe 18 Agosti mwaka 2023 kuanzia saa 2 kamili asubuhi katika ukumbi wa Naivera Complex Limited jijini Tanga.

Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein M. Bashe (MB). Mada mbalimbali zinazohusu maendeleo ya tasnia ya korosho nchini zitawasilishwa na kujadiliwa.

Barua za mwaliko zimetumwa kwa Waalikwa wote. Waalikwa wanaombwa kujigharamia kuhudhuria mkutano huo kwa usafiri, malazi na gharama zingine. Bodi ya korosho itagharamia chai, kabrasha la mkutano, chakula pamoja na viburudisho wakati wote wa Mkutano.

Aidha, mkutano huu ni kwa wadau waliopata barua za mwaliko pekee. Kila mshiriki afike na barua yake ya mwaliko pamoja na kitambulisho chake. Asiye na barua ya mwaliko hataruhusiwa kushiriki mkutano huo.

**Tangazo hili limetolewa na:**
**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
**S. L. P. BOX 533.**
**MTWARA**

IDT INLAND DEVELOPMENT TANZANIA

## INLAND DEVELOPMENT TANZANIA

DIOCESE OF TABORA
P.O. BOX 1286
TABORA, Tanzania, E.A
Bishop +255 786854375
General Secretary +255 784219232
Office Tel. +255 732 988 862
Email- aict.tabora@gmail.com

## NOTICE OF TENDER

**RFQ Title:** Supply of Tablets
**Date of solicitation:** 01/08/2023
**Submission Date and time:** 15/08/2023- 16:00 P.M Hrs.
**Question & clarification:** 5/08/2023

**Introduction**

INLAND DEVELOPMENT TANZANIA (IDT) is a Non - Governmental Organization legally registered under the Act NO. 24 of 2002 on August 2019 with registration NO. 00NGO/R/0489 to operate in Tanzania Mainland. Inland Development Tanzania (IDT) Diocese of Tabora is the inheritor name of African Inland Church Tanzania (AICT), which was a Faith Based Organization (FBO) and non-profit organization. The organization's head office is located in Tabora Municipal at AICT Diocese of Tabora, opposite the JB series Hotel. IDT is currently implementing programs in the Tabora region and has sub-offices in each council of the Tabora region.

IDT aims to develop endeavors and empower the community to overcome poverty, Ignorance, and diseases and advocate for human rights.

With this support from CNHF, Pact in collaboration with IDT integrate Early Childhood care and development activities into the ACHIEVE project. The ACHIEVE project, which is led by Pact and funded by PEPFAR through USAID, aims to improve the health and well-being of orphans and other vulnerable children (OVC), with a focus on children and adolescents living with or most at risk of contracting HIV and their caregivers. Through ACHIEVE, Pact delivers home-based, child-centered case management services, in line with Tanzania's National Integrated Case Management System (NICMS), Conducting service training in community education on adolescent, peadtric Health and Nutrition for under five years, Data review Meetings, Bi-annual Data Summit, CCW's and LV monthly meeting, Education subsidies distribution and normal field supportive supervision, CHMT Meeting, Clinical Home visiting and supportive supervision to high volume CTC to all councils. Conducting in service training in community education on adolescent, peadtric Health and Nutrition to under three years.

**Items specification and requirements**

| Quantity | Specifications | Other | Quantity | Estimated Time of Delivery |
|---|---|---|---|---|
| 275 Tablets | • Build: Aluminum body<br>• Display: 8.7"<br>• Internal memory: at least 32GB<br>• RAM: at least 4 GB<br>• CPU: Octa-core (4x2.3 GHz Cortex-A53 & 4x1.8 GHz Cortex-A53)<br>• Chipset: Mediatek MT8768T Helio P22T (12 nm)<br>• Network: GSM/HSPA/LTE<br>• OS: At least Android 11<br>• Battery: Non-removable Li-Ion 5100 mAh battery | • Built in camera: 8 MP<br>• Resolution: 800 x 1340 pixels, 5:3 ratio (~179 ppi density)<br>• Wi-Fi 802.11 a/b/g/n/ac, dual-band, Wi-Fi Direct<br>• Dedicated microSD Card slot<br>• USB: USB Type-C 2.0<br>• GPS, GLONASS, BDS, GALILEO | • 275 | • 6 days |
| Screen protectors and covers | • Glass screen protector<br>• Silicon cover | | | |

**Eligibility**

Vendor must be currently operating in Tanzania and the Quotation must include all the following information

- Ability to meet the above specification
- Ability to deliver the items within the specified time.

**Evaluation Criteria**

- Price
- Delivery Time
- Experience
- Quality of items that will be supplied
- Financial stability
- Eligibility

**The following should be included in the application**

- Drafted inception explaining the methodology to supply the items
- Quote, Valid for at least 90 days
- Current company files
- Copies of Office registration certificates and address, valid business licenses, VAT, TIN certificates, and Tax clearance.
- Items of the specification are explained in the above table.
- Current audited Financial Statements.
- Original bank statement for the past 12 months.
- Delivered time must be specified.
- Payment terms 100% after delivery.
- Evidence for similar items/services and at least two (2) names of clients served with their addresses.

**All interested bidders should access and download full terms of reference via AICT Website, www.aictanzania.org**
**All questions and clarification should be directed to procurement@idt.or.tz with the subject "Tender Clarification"**

**How to submit:**

- Bids should be submitted in an enclosed and sealed envelope.
- The eligible vendors should physically submit their proposal to the Tender committee, P.O. Box 1286 IDT TABORA.
- All quotes must be in Tanzanian shillings and enclosed in a plain sealed envelope.
- The deadline for proposal submission will be August 15th, 2023 at 16:00 PM, and IDT will open the bids on August 16th 2023 10:00 AM.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wajasiriamali wasikatishwe tamaa, bidhaa zao zinunuliwe

**TAKWA** la Sheria ya Ununuzi wa Umma nchini linaelekeza kutengwa asilimia 30 ya bajeti kwa ajili ya kununua bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo badala ya kiasi chote kutumia kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi.

Sheria hii imezingatia umuhimu wa kuwajali wazalishaji wa kitanzania kwa kununua bidhaa wanazozitengeneza ili kuthamini kinachotengenezwa ndani ya nchi.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wakuu wa taasisi zote za serikali kutekeleza takwa la sheria ya manunuzi ya umma nchini linaloelekeza kutengwa kwa asilimia 30 ya bajeti za manunuzi kwa ajili ya kununua bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamli wadogo badala ya kiasi chote kutumika kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi.

Hiyo pia itasaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira ambalo limekuwa kubwa nchini kutokana na vijana wengi wanaomaliza elimu za juu kuhaha kutafuta ajira hasa serikalini.

Sekta ya ujasiriamali imekuwa mkombozi mkubwa kwa sababu wengi wa vijana hao wanapohitimu masomo yao huamua kujiajiri wenyewe. Katika sekta hiyo imeonekana kuwa Watanzania wana ubunifu mkubwa wa kutengeneza bidhaa zenye viwango vya hali ya juu, lakini tatizo linakuja kwenye soko.

Kama Watanzania wangekuwa na utamaduni wa kuthamini bidhaa zinazozalishwa nchini, basi sekta hiyo ingekuwa na kuondoa kabisa tatizo la ajira hasa kwa vijana.

Duniani kote tatizo la ajira ndiyo kilio cha vijana wengi na kusababisha wanaotoka nchi zinazoendelea hasa Afrika kukimbilia Ulaya au Marekani ili waweze kujinasua katika tatizo hilo.

Kwa upande wa serikali inatekeleza miradi mingi ikiwamo ya ujenzi wa shule, miji na tunatumia fedha nyingi kuagiza bidhaa nje ya nchi wakati wapo wajasiriamli ambao wanazalisha bidhaa kama vile gypsum, lakini zinaagizwa kutoka China.

Kama serikali iliweza kudhibiti ununuzi wa samani kutoka nje ya nchi, hata bidhaa nyingine zinaweza kudhibitiwa ili kuwapa fursa wazalishaji wa ndani. Tukiangalia samani zilizokuwa zikiagizwa toka nje hazikuwa na ubora kama zinazotengenezwa ndani na matokeo yake baada ya muda zinaharibika na kununuliwa nyingine.

Tanzania ina utajiri mkubwa wa malighafi za kutengenezea samani bora kutokana na kuwa na miti ya aina tofauti ya kuzalisha mbao bora.

Kuna mawe mazuri ambayo huzalisha marumaru nzuri zenye ubora wa hali ya juu, lakini kwa kutothamini cha kwetu, mtu anakwenda China anaagiza kasha zima la bidhaa hiyo kwa ajili ya nyumba yake.

Serikali imezitaka taasisi za serikali kuzingatia sheria hiyo ya ununuzi wa umma kwa kutenga fedha kwa ajili ya kununua bidha zinazozalishwa na vijana wa kitanzania.


aliwataka vijana kuchangamkia fursa zilizopo kujiajiri kwa kubuni miradi mbalimbali itakayo waingizia kipato na kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

Pia Watanzania hasa kundi la vijana linatakiwa kutumia fursa hiyo ya ujasiriamali kujiajiri badala ya kusubiri ajira za serikali.

Vijana wengi wamefanikiwa kwa kuanzisha miradi yao ya ujasiriamali na wao kutoa ajira kwa wenzao na sasa wanamaendeleo makubwa. Halmashauri zote nchini zina wajibu wa kutenga maeneo ili vijana wayatumie katika shughuli mbalimbali za uzalishaji kama vile kilimo na kuwaunganisha na fursa za kupata zana bora za kilimo, mbegu bora na kuacha tabia ya kusubiri kilimo cha msimu wa mvua na kujikita katika kilimo cha umwagiliaji ili waweze kupata tija.

Kutokana na serikali kuwajali vijana, imewataka walio tayari kufanya uwekezaji katika sekta mbalimbali wasaidiwe kupata fursa zinatolewa na serikali na kuwekewa mazingira mazuri ya uwekezajii ili kutimiza ndoto zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Madereva wazingatie agizo la Majaliwa waache 'kupiga nyoka'

Na Adam Fungamwango

**AKIKABIDHI** magari 30 na vitendea kazi vya kupima afya na usalama mahali pa kazi na kwa ofisi za mikoa, Idara ya Kazi na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alikemea wizi wa mafuta kwa madereva wa magari ya serikali.

Akiwa jijini Dodoma, Waziri Mkuu alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya madereva kujihusisha na wizi wa mafuta kupitia vituo vya mafuta au kutoka katika magari yao.

"Nawaagiza maofisa na vyombo vya usalama wahakikishe wanafanya ufuatiliaji kikamilifu kuchukua hatua kuhusu taarifa za baadhi ya madereva wanaojihusisha na wizi wa mafuta kupitia vituo vya mafuta au katika magari," alisema Waziri Mkuu.

Licha ya kuagiza mambo kadhaa, hili la wizi wa mafuta haliwezi kuondoka hivi hivi bila ya kuongelewa. Kwa muda mrefu baadhi ya madereva, sio wa serikali, hata wa mashirika ya umma na idara zake, makampuni na watu binafsi wamekuwa na tabia hiyo ambayo pamoja na kwamba inaathiri utendaji wa kazi, lakini pia inazitia hasara serikali na taasisi hizo za watu binafsi.

Baadhi yao wasiyo waaminifu baada ya kujaziwa mafuta na kukabidhiwa magari wanakuwa na wateja wao ambapo wanakwenda sehemu ambayo imetengwa kwa ajili hiyo na kunyonya kutoka kwenye magari hayo na kuingiza kwenye vidumu na baadaye kuuziana na wanayoyahitaji.

Wenyewe madereva wenye tabia hiyo wana msamiati wao wanaita 'kupiga nyoka.'

Neno hilo lina maana ya kwamba ule mpira wa plastiki unaotumika kuingizia kwenye mdomo wa tanki ya mafuta na kunyonya, unaitwa 'nyoka.'

Vitendo hivi vinafanywa kwa siri sana na baadhi ya madereva wanafanya hivyo kwa ajili ya kujipatia kipato cha ziada kwa sababu anakuwa amejaziwa bure kwa ajili ya kuyafanyia kazi iliyokusudiwa.

Kama alivyosema Waziri Mkuu, vitendo hivyo wala huwezi kuvipa jina lolote zaidi ya wizi, kama wizi mwingine wowote ule.

Kwa sababu baada ya muda serikali inabidi iingie tena hasara ya kujaza mafuta, kumbe haikupaswa kufanya hivyo kwa muda mfupi huo.

Idadi ya madereva wanaofanya hivyo inaongeza pia idadi ya mafuta yanayoibiwa.

Pamoja na kwamba, Mheshimiwa Majaliwa amewasema madereva wa serikali, lakini liende pia kwa madereva wote nchini wanaoendesha magari ya taasisi za serikali na binafsi.

Ifike wakati baadhi ya madereva watosheke na vipato wanavyovipata na kutafuta njia nyingine halali ya kujitafutia kipato cha ziada kwa sababu nchi yetu kwa sasa haijakataza mtu yoyote kujitafutia pesa nje ya kazi yake 'mama', ili mradi tu iwe halali.

Kitendo chochote wanachofanya cha wizi wa mafuta, iwe kunyonya kwenye madumu na kuuza kwenye watu binafsi au vituo vya mafuta, au kudanganya taarifa za umbali ni hujuma, na zinatakiwa kuachwa, lakini wale wanaopatikana ni lazima wapewe adhabu.

Tayari Waziri Mkuu amekemea na ameshaagiza vyombo vya usalama kufanya kazi yake, ina maana wale watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria na kinidhamu pia, hivyo ni wakati sasa wa kurekebisha tabia.

Siyo kwa madereva wa serikali bali wote kwa sababu wanayopata serikali ndiyo wanazopata sekta binafsi pia.

Pesa zinazonunuliwa mafuta ya ziada kufidia yale ambayo wameibiwa zingeweza kufanya kitu chochote kile cha manufaa kwa watu wengine kama vile kulipa mishahara kwa wakati, au kutoa matibabu kwa wafanyakazi ambao wamepatwa matatizo kazini. Nadhani madereva wote wamemsikia Waziri Mkuu, ni wakati wa kuacha 'kupiga nyoka' kwa wenye tabia hiyo na kuwa waadilifu kwenye kazi zao.

## Wakulima waishukuru CRDB mikopo zana za kilimo, mitaji

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BAADHI ya wakulima mkoani Mbeya wameishukuru Benki ya CRDB mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia mikopo ya fedha na nyenzo ikiwamo trekta aina ya power tiller.

Wamesema zana hizo zitawasaidia kuinua kilimo na kukuza mapato yao na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mmoja wa wakulima hao kutoka Wilaya ya Mbalali, mkoani Mbeya, Halima Ally, alitoa ushuhuda huo juzi mbele ya Rais Samia, alipotembelea banda la CRDB kwenye Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

"Sisi wakulima wa Mbarali tunaishukuru Benki ya CRDB kwa kutuwezesha kupata mikopo ya fedha na zana za kufanyia kazi kama ilivyotukopesha power tiller. Kwa kupata Power Tiller hii, itaniwezesha kuendeleza kilimo changu cha mpunga na mahindi," alipongeza Halima.

Wakulima zaidi ya 600 kutoka Wilaya ya Mbarali wanatarajiwa kukopeshwa na Benki ya CRDB trekta, power tiller, zana za kuvunia, fedha za mikopo ya kulimia na pembejeo za kilimo zikiwamo mbegu, mbolea na dawa pamoja na mikopo kwa ajili ya stakabadhi ghalani.

Rais Samia aliipongeza Benki ya CRDB kwa kukopesha wakulima kwa riba ya asilimia tisa, huku akiitaka kuendelea kufuatilia zana za kilimo wanazowakopesha wakulima ili ziendelee kufanya kazi na ikibidi kuwasaidia kutengeneza pindi zinapoharibika kwa kuwa baadhi yao zana hizo zikiharibika, wanazitelekeza.

"Ninawapongeza CRDB kwa kutoa mikopo ya riba ya asilimia tisa. Itawasaidia wakulima kukopa kwa wingi na kulima kwa tija.

"Na mikopo ya power tiller mnayotoa kwa wakulima fuatilieni na kuwasaidiia (wakulima) waweze kutengeneza. Wakati mwingine power tiller linaharibika na kulitelekeza, hivyo kushindwa kuleta tija," aliagiza Rais Samia.

Mkuu wa Kitengo cha Kilimo Biashara wa Benki ya CRDB, Maregesi Shaaban, alisema Benki ya CRDB imeendelea kutoa mikopo inayofikia Sh. trilioni 3.9 kwa misimu mitano iliyopita hadi kufikia Julai 2023, sawa na asilimia 43 ya mikopo yote itolewayo na benki katika sekta za kilimo na mifugo nchini.

"Tunatoa mafunzo kwenye vituo atamizi chini ya mpango maalum wa BBT kupitia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Tunaendelea kutoa elimu ya fedha na usimamizi wa miradi kwenye vituo vilivyoko kote nchini," alisema.

Alisema Benki ya CRDB kupitia kampuni yetu tanzu ya CRDB Bank Foundation, inawekeza kwa vijana na wanawake ili watimize ndoto zao kwa kuwapa mafunzo na kuwapatia mitaji kwa ajili ya uanzishaji wa miradi mipya.

Mitaji hiyo hutolewa kwa vijana na wanawake wenye mawazo bunifu kibiashara na Benki ya CRDB inatoa mitaji ya awali ikiwa ni mbegu itakayoleta matunda na kuwafungulia kesho yao yenye tija zaidi kiuchumi, chini ya programu ya IMBEJU.

"Benki ya CRDB itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuendeleza fursa za uwekezaji zilizopo Tanzania Bara na Visiwani (Tanzania Zanzibar)," alisema.

Aliwakabirisha wadau wote waliopo ndani na nje ya nchi ya Tanzania wafike katika matawi ya benki hiyo yaliyoko nchini na nchi jirani za Burundi na Congo DRC ili wapatiwe huduma.



Mzee Mohamed Muhaba, akionyesha jengo la ofisi ya serikali ya Kitongoji cha Kikonga, Kata ya Bupu wilayani Mkuranga mkoani Pwani juzi, ambalo ni la muda mrefu na limechakaa hivyo kuiomba serikali kuwajengea jengo jipya na kisasa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hukumu kesi kupinga mkataba Bandari leo

**Na Kulwa Mzee,** MBEYA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Mbeya leo inatarajia kutoa uamuzi wa kesi ya kupinga mkataba unaolenga kuendesha, kuwekeza na kuendeleza bandari nchini baada ya kukwama kufanya hivyo Agosti 7, mwaka huu.

Uamuzi wa shauri hilo ulipangwa kusomwa leo mbele ya jopo la majaji watatu; Jaji Dunstan Ndunguru, Jaji Mustafa Ismail na Jaji Abdi Kagomba.

Agosti 7, mwaka huu, Msajili wa Mahakama Kuu, Projest Kahyoza, akiahirisha shauri hilo, alisema mara ya mwisho baada ya pande zote mbili kukamilisha kuwasilisha hoja, mahakama ilipanga uamuzi utolewe tarehe hiyo.

"Mwenyekiti wa Jopo la Jaji Dunstan Ndunguru kapata dharura, jopo walikubaliana wasome uamuzi wakiwa pamoja, kwa tarehe itakayopangwa mwenyekiti atakuwapo, shauri linaahirishwa hadi Agosti 10 mwaka huu saa tatu asubuhi," alisema Msajili Kahyoza alipoliahirisha shauri.

Uamuzi wa shauri hilo utasikilizwa katika kumbi mbili kwa kuwa wasikilizaji watakuwa wengi, ukumbi wa mahakama Na. 4 na ukumbi wa pili wananchi watasikiliza kupitia video.

Shauri hilo lilifunguliwa na wanasheria watatu kutoka mikoa tofauti; Alphonce Lusako, Emmanuel Chengula, Raphael Ngonde na Mwananchi Frank Nyalus . Wanasheria hao walifungua kesi dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Katibu wa Bunge la Tanzania, ambaye ni mtendaji mkuu na mratibu wa shughuli za Bunge.

Walalamikaji wanawakilishwa na Mawakili Mpale Mpoki, Boniface Mwabukusi, Livino Ngalimitumba na Philipo Mwakilima.

Pande zote mbili katika shauri hilo zilikubaliana kwamba hoja sita ndizo zinazobishaniwa mahakamani ambapo wananchi na walalamikaji wanatarajiwa kupata uamuzi wa mahakama kuhusiana na hoja hizo.

Hoja hizo ni kama kutia

Pande zote mbili katika shauri hilo zilikubaliana kwamba hoja sita ndizo zinazobishaniwa mahakamani; ya kwanza ni kama kutia saini, kuwasilisha bungeni na kuridhia mkataba wa Tanzania na Dubai kulikiuka kifungu cha 11(2), Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Raslimali na Maliasili, Sheria Na. 5 ya Mwaka 2017 kikisomwa pamoja na Sheria ya Mapitio na Majadiliano ya Mikataba ya Masharti Hasi, Sheria Na. 6 ya Mwaka 2017. Hoja ya pili ni kama umma uliarifiwa na kupewa muda mwafaka kushiriki na kutoa maoni yao kama sheria zinavyotaka kuhusiana na utaratibu wa kupitisha na kuridhia mikataba.

Katika shauri hilo, hoja ya tatu ni kama ibara ya 2, 4(2) zinakiuka Ibara namba 1,8 na hoja ya nne, kama IGA kati ya Tanzania na Dubai ni mkataba na hoja ya tano kama Ibara ya 2 na 23 za IGA zinakiuka kifungu cha 25 cha Sheria za Mikataba Tanzania.

Hoja ya sita inayobishaniwa ni kama IGA kati ya Tanzania na Dubai ilifuata taratibu za kisheria katika kuchagua njia ya zabuni ambazo zimewekwa chini ya kifungu cha 64 cha Sheria ya Ununuzi.

Kiongozi wa jopo la mawakili wa serikali, Wakili wa Serikali Mkuu, Mark Mlwambo awali aliweka pingamizi dhidi ya shauri hilo, akiomba mahakama itupilie mbali. Alitoa sababu nne, lakini Julai 25 mwaka huu upande wa serikali uliamua kuondoa pingamizi.

Wakili Mlwambo akiwasilisha hoja za kuomba kuondoa pingamizi akidai sababu kubwa ni kupisha usikilizwaji wa shauri mama na hakuna gharama kwa upande wowote.

Wakili Mpale Mpoki, akiwawakilisha walalamikaji, alikubaliana na hoja ya serikali kuondoa pingamizi, pia walijadiliana na wateja wao ambapo nao walikubaliana wakiwa na lengo la kuharakisha usikilizwaji na uamuzi wa shauri la msingi.

Walalamikaji katika shauri hilo wanapinga makubaliano yanayohisha uwekezaji katika bandari za Tanzania zilizoko katika mwambao wa bahari na katika maziwa, kuwa ni batili kwa kuwa yana ibara zinazokiuka sheria na Katiba ya nchi.

Wanadai makubaliano hayo yanahatarisha mamlaka ya nchi na usalama wa taifa na yaliridhiwa na Bunge kinyume cha utaratibu bila kuwapa nafasi ya kutosha wananchi kutoa maoni yao.

Makubaliano hayo yalitiwa saini Oktoba 25, 2022 na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, baada ya kupewa nguvu ya kisheria na Rais Samia Suluhu Hassan, huku Katibu Mkuu wa wizara hiyo, akishuhudia na yaliridhiwa na Bunge Juni 10, 2023.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa Julai 25 mpaka Julai 28 mwaka huu, mawakili wa waombaji katika shauri hilo walipomaliza kuwasilisha hoja zao huku wakidai mkataba umekiuka sheria na Katiba ya nchi.

## KABWELA  Na Fadhili Mohammed



# THE MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY

THE MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY

## FACULTY OF LEADERSHIP AND MANAGEMENT SCIENCES DEPARTMENT OF LEADERSHIP, ETHICS AND GOVERNANCE LEADERSHIP AND ETHICS SHORT COURSES FOR 2023/2024

| | Course | Duration | Training Centers | Dates | Costs TZS |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Short Courses For Senior Public Leaders: Permanent Secretaries, Heads of Departments, Heads of Units and Heads of Public Institutions)** | | | | |
| 1 | Ethical Leadership in the Public Service | 3 Days | Kivukoni DSM | 19th -21st Sept. 2023 | 750,000 |
| 2 | Professionalism in the Public Service | 3 Days | Kivukoni DSM | 26th -28th Sept. 2023 | 750,000 |
| 3 | Building an Effective Public Service Management System | 3 Days | Zanzibar | 3rd -5th Oct. 2023 | 750,000 |
| 4 | Participatory Public Service Delivery | 3 Days | Zanzibar | 10th-12th Oct. 2023 | 750,000 |
| 5 | Strategic Human Resource Management in the Public Service | 3 Days | Zanzibar | 24th -26th Oct. 2023 | 750,000 |
| 6 | Leadership Entrepreneurship, Creativity and Innovation | 4 Days | Kivukoni DSM | 06th -09th Nov. 2023 | 750,000 |
| 7 | Emotional Intelligence | 3 Days | Kivukoni DSM | 14th -16th Nov. 2023 | 750,000 |
| | **Short Courses for the Chief Executive Officers (CEOs) and Executives** | | | | |
| | Leadership and Ethics in Business Environment | 4 Days | Zanzibar | 20th -23rd Nov. 2023 | 900,000 |
| 2 | Building an Effective Corporate Management System | 4 Days | Zanzibar | 27th -30th Nov. 2023 | 900,000 |
| 3 | Corporate Competitive Strategy | 4 Days | Kivukoni DSM | 5th -8th Dec. 2023 | 900,000 |
| 4 | Networking and Strategic Communication | 3 Days | Kivukoni DSM | 12th -14th Dec. 2023 | 850,000 |
| | **Short Courses for Local Government Leaders** | | | | |
| 1 | Fundamentals of Local Governance | 3 Days | Zanzibar | 19th -21st Dec, 2023 | 450,000 |
| 2 | Performance Management at the Local Level | 4 Days | Zanzibar | 8th -11th Jan, 2024 | 450,000 |
| 3 | Community Engagement | 4 Days | Kivukoni DSM | 13th -16th Jan, 2024 | 500,000 |
| 4 | Entrepreneurship at Local Government Level | 3 Days | Kivukoni DSM | 20th -22th Jan, 2024 | 450,000 |
| 5 | Managing Human Resources at The Local Level | 4 Days | Zanzibar | 26th -29th Jan, 2024 | 500,000 |
| 6 | Ethical Elections Monitoring | 3 Days | Kivukoni DSM | 6th -8th Feb, 2024 | 450,000 |
| 7 | Small Business Ethical Management | 3 Days | Kivukoni DSM | 20th -22nd Feb, 2024 | 450,000 |
| | **Short Courses for Diplomatic Community** | | | | |
| 1 | Introduction to International Relations and Global Politics | 3 Days | Kivukoni DSM | 27th -29th Feb, 2024 | 900,000 |
| 2 | International Law and Diplomacy | 3 Days | Zanzibar | 5th -7th March, 2024 | 900,000 |
| 3 | Conflict Resolution and Peacekeeping | 3 Days | Zanzibar | 12th -14th March, 2024 | 900,000 |
| 4 | Global Security Issues | 3 Days | Kivukoni DSM | 19th -21th March, 2024 | 900,000 |
| 5 | Regional Dynamics and Geopolitics | 3 Days | Kivukoni DSM | 26th -28th March, 2024 | 900,000 |

| | Course | Duration | Training Centers | Dates | Costs TZS |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Short Courses on Peace Building and Conflict Resolution for Defence, Inteligence and Police Officers** | | | | |
| 1 | Introduction to Peace Building Strategies | 3 Days | Zanzibar | 2nd -4th April, 2024 | 750,000 |
| 2 | Analysis of Conflicts in Great Lakes | 3 Days | Zanzibar | 9th -11th April, 2024 | 750,000 |
| 3 | Approaches to Conflict Resolution | 3 Days | Kivukoni DSM | 16th -18th April, 2024 | 750,000 |
| 4 | Post - Conflict Interventions with Gender Perspective | 3 Days | Kivukoni DSM | 23rd -25th April, 2024 | 750,000 |
| | **Short Courses on Organizational Communication for Personnel and Managers** | | | | |
| 1 | Organizational Communication | 3 Days | Kivukoni DSM | 7th – 9th May, 2024 | 500,000 |
| 2 | Communication Strategies in Organisations | 3 Days | Kivukoni DSM | 14th – 16th May, 2024 | 500,000 |
| 3 | Intercultural Communication in Organizations | 3 Days | Kivukoni DSM | 21st – 23rd May, 2024 | 500,000 |
| 4 | Organizational Conflict Resolution and Negotiation | 3 Days | Kivukoni DSM | 28th – 30th May, 2024 | 500,000 |
| 5 | Communication Technologies in Organisations | 3 Days | Kivukoni DSM | 4th – 6th June, 2024 | 500,000 |
| | **Short Courses on Gender and Leadership for Governmental and Non Governmental Stakeholders** | | | | |
| 1 | Introduction to Gender and Leadership | 3 Days | Zanzibar | 4th – 6th June, 2024 | 750,000 |
| 2 | Gender Theoretical Perspectives and integration in leadership | 3 Days | Zanzibar | 11th – 13th June, 2024 | 750,000 |
| 3 | Gender Bias and Stereotyping in organizational Leadership | 3 Days | Kivukoni DSM | 18th – 20th June, 2024 | 750,000 |
| 4 | Women in Poilitical Leadership:Challenges and Opportunities | 4 Days | Kivukoni DSM | 25th – 28th June, 2024 | 800,000 |
| 5 | Men as Allies in Gender and Leadership | 3 Days | Zanzibar | 2nd -4th Jul, 2024 | 750,000 |
| 6 | Leadership Development for Gender Mainstreaming | 3 Days | Zanzibar | 9th -11th Jul, 2024 | 750,000 |
| | **Short Courses for Leadership in the Digital Era** | | | | |
| 1 | Introduction to Leadership in the Digital Era | 3 Days | Zanzibar | 16th -18th Jul, 2024 | 900,000 |
| 2 | Digital Strategy and Innovation | 3 Days | Kivukoni DSM | 23rd -25th Jul, 2024 | 900,000 |
| 3 | Leading Teams in the Digital Era | 3 Days | Kivukoni DSM | 6th -8th Aug, 2024 | 900,000 |
| 4 | Data-Driven Decision Making | 3 Days | Zanzibar | 13th -15th Aug, 2024 | 900,000 |
| 5 | Digital Marketing and Customer Engagement | 3 Days | Zanzibar | 20th -22th Aug, 2024 | 900,000 |
| 6 | Ethics and Digital Leadership | 3 Days | Kivukoni DSM | 27th -29th Aug, 2024 | 900,000 |

# TANGAZO

| | Short Courses for Members of Parliament and Councilors | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Government Oversight Roles and Strategies | 3 Days | Dodoma | 3rd – 5th Sept, 2024 | 900,000 |
| 2 | Anti-Corruption Strategies in Public funded Projects | 3 Days | Dodoma | 10th – 12th Sept, 2024 | 900,000 |
| | **Short Courses for NGOs Leaders** | | | | |
| 1 | NGO's Ethical Leadership | 3 Days | Zanzibar | 19th -21st Sept. 2023 | 500,000 |
| 2 | Local Legal Frameworks | 3 Days | Kivukoni DSM | 26th -28th Sept. 2023 | 500,000 |
| 3 | NGO's Sustainability and Prosperity | 3 Days | Kivukoni DSM | 3rd -5th Oct. 2023 | 500,000 |
| 4 | Human Resource and Volunteer Management | 3 Days | Zanzibar | 10th12th Oct. 2023 | 500,000 |
| 5 | Networking and Strategic Communication | 3 Days | Zanzibar | 24th -26th Oct. 2023 | 500,000 |
| | **Short Courses for Young Leaders and College Students** | | | | |
| 1 | Patriotism and Tanzanian History | 3 Days | Kivukoni DSM | 18th – 20th June, 2024 | 150,000 |
| 2 | Ethical Leadership and Good Governance | 3 Days | Zanzibar | 25th – 27th June, 2024 | 150,000 |
| 3 | Leadership and Entrepreneurship | 3 Days | Kivukoni DSM | 25th – 27th June, 2024 | 150,000 |
| | **Short Courses for Educational Leaders and Administrators** | | | | |
| 1 | Tanzania Education Philosophy and implementation context | 3 Days | Zanzibar | 21st -23rd Nov. 2023 | 500,000 |
| 2 | Leadership and Educational Management | 3 Days | Zanzibar | 28th -30th Nov. 2023 | 500,000 |
| 3 | Educational Policy and Governance | 3 Days | Zanzibar | 5th -7th Dec. 2023 | 500,000 |
| 4 | Curriculum Development and Instructional Leadership | 3 Days | Zanzibar | 12th -14th Dec. 2023 | 500,000 |
| 5 | Technology Integration in Education | 3 Days | Kivukoni DSM | 21st -23rd Nov. 2023 | 500,000 |
| 6 | Curriculum Design, Assessment and Evaluation | 4 Days | Kivukoni DSM | 4th – 7th June, 2024 | 600,000 |
| 7 | Educational Equity and Inclusion | 3 Days | Kivukoni DSM | 11th – 13th June, 2024 | 500,000 |
| 8 | Education Participatory Planning | 3 Days | Kivukoni DSM | 18th – 20th June, 2024 | 500,000 |
| 9 | Leading with Emotional Intelligence | 3 Days | Kivukoni DSM | 25th – 27th June, 2024 | 500,000 |
| 10 | Education resource Management and Accountability | 4 Days | Kivukoni DSM | 2nd -5th Jul, 2024 | 600,000 |
| 11 | Cross - cutting issues and Gender Based budgeting in Education | 3 Days | Kivukoni DSM | 3rd – 5th Sept, 2024 | 500,000 |
| 12 | Strategies for managing Development partners in Education | 3 Days | Kivukoni DSM | 10th – 12th Sept, 2024 | 500,000 |

****Training centres/venues and dates can be organised depending on the needs of the client**

****The cost covers Tuition Fee, Handouts, Health Break Tea, Lunch, and Certificate**

**Application and Enrollment Information**

To secure your spot in this transformative Ethical Leadership Short Courses, visit our website at **www.mnma.ac.tz** or call us at **022 2820041/2820047**

**How to Pay**

1. Via Bank: Visit any Branch or Bank agent of NMB, CRDB Rereference No **994120316078**


2. Via Mobile Network Opertors (MNO).
   - Enter to the respective USSD Menu of MNO
   - Select 4 ( Make Payments)
   - Select 5 (Government Payments) Enter **994120316078** as Reference Number

**Direct Contacts**

**Dr. Angela M. Kavishe**
Head of Department- Leadership, Ethics and Governance **MOBILE: +255 754215738**
**amkavishe@gmail.com**
**angela.kavishe@mnma.ac.tz**

**Dr. Adili Zella**
Dean- Faculty of Leadership and Management Sciences
+255 787260448
**zellahadil@gmail.com**

217541902



HABARI KANDA YA ZIWA

# Shirika laokoa wananchi kutumia maji na wanyama

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAKAZI zaidi ya 30,000 kutoka kata tatu za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mkoani hapa, wameondokana na tatizo la kutumia maji na mifugo baada ya Shirika la Kimataifa la LifeWater International la Marekani kutekeleza miradi ya maji awamu ya kwanza.

Wakazi hao kutoka kata za Mwantini, Mwalukwa na Mwamala. Awali walikuwa wanatumia maji ya kwenye visima na mabwawa ya kunyweshea mifugo yao hali ilikuwa inawapa magonjwa.

Wakizungumza na Nipashe, mkazi wa Kata ya Mwalukwa Agnes Musa alisema kuwa kabla ya kuwepo kwa miradi hiyo ya maji walikuwa wakitumia muda mrefu kufuata huduma hiyo ya majina na kushindwa kufanya shughuli zao za kimaendeleo.

Kadhalika, alisema kuwa licha ya kufuata maji hayo mbali vilevile yalikuwa machafu na kuhatarisha afya zao ikiwa ni pamoja na kusababisha magojwa ya mlipuko.

Naye Juma Ramadhani alisema wakati wa kiangazi visima na mabwawa waliyochimba yalikauka na walihangaika kupata maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na mifugo.

Akizungumza juzi alipotembelea baadhi ya miradi ya maji inayotekelezwa na Shirika la Life Water International kushirikiana na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkurugenzi wa LifeWater Tanzania, Devocatus Kamara alisema, mradi huo unathamani ya Sh. bilioni moja.

Kadhalika, alisema miradi hiyo inajumuisha ujenzi wa vyoo bora na mifumo ya maji safi na salama katika baadhi ya shule za misingi ili kuwaondolea adha ya kutafuta maji wakati wa masomo na kusababisha kukosa vipindi wakati wakiwa shuleni.

Alisema, wamefanikisha kufikisha huduma ya majisafi na salama kuanzia asilimia 34 hadi asilimia 75 kwa awamu ya kwanza ya mradi na wataendelea na miradi hiyo ili kuhakikisha huduma inawafikia wananchi na kuwataka wananchi kuitunza ili iwanufaishe wote na wale watakaobainika kuihujumu wafichuliwe.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Shinyanga, Emael Nkopi alisema, wamekuwa wakitekeleza miradi ya maji kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

Alisema awamu ya kwanza wakazi wa Kijiji cha Bulambila Kata ya Mwantini na wanafunzi wa Shule ya Msingi Hinduki wameanza kutumia maji safi na salama na sasa hawachangii maji na wanyama.

## Askofu akemea vitendo vya uhalifu, ushoga kwa vijana

**Na Samson Chacha,** TARIME

ASKOFU wa Kanisa la EAGT Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Joshua Maswi amewaasa vijana kutojiingiza katika vitendo vya uhalifu, matumizi ya dawa za kulevya, unyang'anyi pamoja na ndoa za jinsia moja.

Amewataka kufanya kazi kwa bidi na kujikomboa kiuchumi.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa mazishi ya Ofisa Mstaafu wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Werema Chacha aliyefariki dunia katika Hospitali ya Rufani Kanda Bugando kutokana na ugonjwa wa moyo.

Alitaja vitendo hivyo kuwa ni kinyume na maadili ya dini pamoja na nchi, huku akiwataka kuacha kuiga kila utamaduni unatoka katika mataifa ya ulaya kwa kile alichokiata kuwa utamaduni mwingine ni upotofu.

"Vijana mnazo fursa nyingi za kuwaingizia kipato na kuwainua kimaisha ikiwa ni pamoja na kilimo, uchimbaji madini na hizi shughuli zote zinawategemea ninyi mziendeshe kwa maendeleo ya baadaye," alisema

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tarime, Thobias Ghati alitoa salamu za rambirambi kwa mjane Merysiana Werema ambaye ni Mwenyekiti wa Kata Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Nyandoto.

Kadhalika, aliwataka vijana kuiga mfano wa uchapakazi wa ofisa huyo aliyelipigania taifa kwa nyakati tofauti alipokuwa jeshini.



Ujumbe kutoka Tume ya Madini ukipatiwa maelezo ya mradi wa kilimo biashara wa vijana kijijini Matongo wilayani Tarime unaotekelezwa na mgodi wa Barrick North Mara, walipotembea mradi huo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tani 634,373 za mazao zavunwa msimu wa 2022/23

**Alex Sayi na Neema Charles** (SAUT)

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla amesema zaidi ya hekta 455,498.05 za mazao zimelimwa katika msimu wa mwaka 2022/23 na kupata mavuno tani 634,373.78 sawa na asilimia 80.

Pia amewataka maofisa ugani kuwafikia wakulima kwa wakati lengo likiwa ni kuongeza uzalishaji katika msimu unaofuata.

Alitoa takwimu hizo juzi wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika mikoa ya Kanda ya Ziwa Magharibi mkoani Mwanza huku kanda ya ziwa mashariki yakifanyika mkoani Simiyu.

Makalla alieleza kuwa takwimu hizo ni kufikia Juni 2023 na kuwataka maofisa ugani katika mikoa ya Kanda ya Ziwa Magharibi kuhakikisha wanawatembelea wakulima na wafugaji ili kuwakumbusha juu ya kuzingatia kanuni bora za kilimo na ufugaji ili kuweza kupata tija kubwa kwenye uzalishaji.

Kadhalika, aliwataka wakulima waliopata elimu kupitia maadhimisho hayo kuendelea kuitumia kufanya mageuzi katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuongeza uzalishaji na kusaidia kukabiliana na baa la njaa.

"Wataalamu msichoke kuwatembelea wakulima na wafugaji na kuwapa ushauri stahiki na katika maeneo yenu ya kazi anzisheni mashamba darasa ili wakulima waendelee kujifunza na kuyaona mafanikio" alisisitiza Makalla.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Emily Kasagara alifafanua kuwa maonesho hayo yamewapa fursa wadau kutoka sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ambazo zinahusisha utafiti, umwagiliaji pamoja na hifadhi za mazao kujifunza kwa vitendo.

"Jumla ya wadau 863 wameshiriki. Idadi hii inajumuisha mamlaka za serikali za mitaa 13, taasisi za serikali 11, taasisi za fedha saba, taasisi za elimu 10, kampuni ya zana za kilimo tisa pamoja na wajasiriamali wakubwa na wadogo 746" alisema.

Huko mkoani Simiyu pia maadhimisho hayo yalihitimishwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme ambapo aliwakumbusha wakulima na wafugaji kufuata ushauri wa wataalamu katika kuhakikisha wanaongeza kiwango cha uzalishaji na siyo kulima kwa mazoea.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa Mkoani Simiyu, Maisha Mtipa aliwataka wakulima, vijana na kinamama wilayani humo kuchangamkia fursa ya kilimo cha kisasa kwa kutumia mbegu zilizofanyiwa utafiti ili kilimo hicho kiwe na tija kwao.

Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, wilayani Maswa, Robert Urasa alisema kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa inaendelea na mkakati wa kuwahamasisha wakulima kulima alzeti ambalo ni mkombozi kwa wakulima.

Pendo Shilima, ambaye ni mkazi wa Mwanza aliieleza Nipashe kuwa maonyesho hayo yamekuwa na tija kwa wakulima hususani katika kujifunza na kupanua wigo wa kibiashara.

ama
ALHAMISI AGOSTI 10, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Kasoro kimfumo zinazomweka hatarini mwandishi wa habari anapokuwa kazini**



Ukurasa 13

Kikundi Daraja Salama kilivyofika kuchangia damu, daktari akiwazawadia somo



Ukurasa 14

**Operesheni ya kuhifadhi misitu kijijini inavyoipatia faida zahanati iliyotimia**

# Ushuhuda wa vita vya Dk. Samia kutanua ulingo wa mbolea nchini

• Mageuzi ya viwanda hadi kwenye udongo shambani

**Na Peter Orwa**

ILIKUWA kwenye maonyesho ya Nanenane mwaka jana, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akaelekeza watumishi wote katika mnyororo wa thamani wa kilimo, kusimamia kwa umakini agizo lake jipya la mpango wa serikali wa utoaji mbolea ya ruzuku.

Juzi akiwa katika viwanja vya John Mwakangale Mbeya, akaendeleza msisitizo kwamba ruzuku hiyo aliyoianzisha mwaka jana ni endelevu, ila inahitaji tathmini ya kina kwenye tija yake.

Kimsingi, ndani ya mazingira ya shamba, tunda la mbolea hubeba sura kuu mbili, katika utendaji shambani ni la mazingira zaidi, hasa inapoboresha udongo, pia tathmini ya yatokanayo na uzalishaji huo inachukua tafsiri ya kiuchumi.

Rais anasema ni aina ya uamuzi wa kiserikali kuhakikisha kuna kuwapo na chakula cha kutosha kitaifa, huku uchumi wa mtu mmoja mmoja nao unaboreka.

Akaeleza kwamba huo ni mwanzo tu, anafafanua mpango wa serikali ni kuanzishwa viwanda vingi vya kuzalisha mbolea nchini na akazigeuzia uso Wizara za Fedha na Kilimo, akiziagiza zihakikishe mbolea zinatoka kwa wakati na kumfikia mkulima.

Pia, anawataka wakulima wajisajili waliko, ili kukidhi mahitaji ya kunufaika na kupata ruzuku inayolengwa serikalini.

Ni matamshi yanayobeba tafsiri pana, kwa kuzingatia sekta ya kilimo inatoa ajira ya moja kwa moja kwa theluthi mbili ya Watanzania, ikimaanisha wastani wa asilimia 65, vilevile kukiwapo asilimia 10 ya kazi zisizo za moja kwa moja, ila zina mzizi utokao kwenye kilimo.



Sehemu ya kiwanda kipya cha mbolea cha Intracom, kilichozinduliwa jijini Dodoma, Desemba mwaka jana. **PICHA: MTANDAO**

Sekta ya Kilimo ambayo Rais Dk. Samia anawekeza nguvu zake, inazalisha asilimia 28 ya pato la taifa, ambayo katika lugha rahisi ni zaidi ya robo la mavuno hayo kwa nchi.

Ni ndani ya mwaka huo, 2022 tangu atoe maagizo, miezi minne baadaye, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akazindua kiwanda cha Mbolea katika eneo la Dodoma, akinena "matamanio ya Rais Samia yafikiwa."

Waziri Mkuu analitolea ufafanuzi kwamba: "Kuna fursa nyingi katika kiwanda hiki ikiwamo upatikanaji wa mbolea ya uhakika na kwa gharama nafuu,"

Majaliwa anakisifu kiwanda hicho kuwa cha kipeke kwa maana ya uzalishaji wake unafanywa kitaifiti, wa kipima mahitaji ya udongo wa mikoa kitaifa na ndio mbolea zinatengenezwa kwa mujibu wa mahitaji kitaifa yaliyotafitiwa.

Hapo Waziri wa Kilimo, Bashe, anaungana na hoja hiyo, akiwa na ufafanuzi kwamba ili kuboresha uzalishaji wa mbolea hizo, serikali imewafutia kodi husika wapate tija ya uzalishaji kwa viwanda vya ndani.

"Katika miongo sita ya uhuru, serikali zote kutoka awamu ya kwanza ya Mwalimu Nyerere, zimekuwa zikitilia mkazo kwa kuanzisha kampeni mbalimbali kama: Kilimo ni Uhai; Kilimo cha Kufa na Kupona; na Kilimo Kwanza," anafafanua Bashe.

Ni mustakabali ambaoMkurugenzi Mkuu wa kiwanda hicho Nduwimana Nazaire, anamwagia sifa Rais Dk. Samia, akimtaja kuwa amewapatia ushirikiano wenye tija katika uzalishaji wao wa mbolea kiwandani.

Ni miezi nane iliyopita wakati wa uzinduzi huo, Nazaire akaahidi kuwa Intraco itakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 600, 000 za mbolea na tani 300,000 za mbolea chokaa.

Bosi huyo msimamizi wa kiwanda hicho kipya kilichoko mkoani Dodoma, pia anawataja wadau wengine wanaowawezesha ni; Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Taarifa ya TFRA inaeleza hadi wakati huo kuna zinduliwa kiwanda cha Dodoma Desemba mwaka jana, kulikuwapo viwanda 13 vya mbolea nchini, zinazozalisha mbolea ngumu na kiminika (za unga), huku vitano vikiwa na miundombinu na mitambo ya kisasa, pia vitatu vinavyozalisha visaidizi vya mbolea.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ana lake la ufafanuzi kwamba kiwanda hicho kipya cha mbolea kilichozinduliwa Dodoma, ni zao la ushawishi wa Rais Dk. Samia katika ziara yake Afrika Mashariki nchini Burundi, kukiwa kumewekezwa Dola za Marekani, milioni 180, na kiwanda kikitarajia kuajiri Watanzania 3,000.

Pia, inafafanuliwa kwamba Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu, Arusha ambacho ni kikongwe, kiko katika maboresho kwa

INAENDELEA UK.13

AFYA

# Kasoro kimfumo zinazomweka hatarini mwandishi wa habari anapokuwa kazini



Waandishi wa habari wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**

**Na Peter Nyanje**

INGAWA inatajwa usalama wa waandishi wa habari nchini umekuwa ukiimarika hivi karibuni, bado kuna haja ya kuwapo na mfumo mahsusi utakaowahakikishia ulinzi wataalamu hao kazini nchini, ili kutimiza majukumu yao katika kuijenga nchi.

Ni mtazamo na utashi wa wadau wa habari yanayobainisha mfumo huo unapaswa kuwa jumuishi, ukiwahusisha wadau mbalimbali wa sekta hiyo.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa Mwanza, Edwini Soko, anashauri umuhimu wa kuwa na mfumo huo, kwa sababu bado waandishi wa habari nchini wanakabiliwa na hatari wanapotekeleza majukumu yao.

"Iwapo mwandishi wa habari atapatiwa ulinzi wa kutosha wakati akifanya kazi zake, basi ataweza kuisaidia nchi kwa ufanisi zaidi kupitia kazi zake," anasema Soko.

Kwa mujibu wa Soko, mfumo huo wa kitaifa unapaswa kuwa na vigezo na kuweka wajibu kwa kila mdau wa habari nchini kuhakikisha anatoa mchango wake kufanikisha ulinzi wa mwandishi wa habari kazini.

Anafafanua, ni mfumo unaopaswa kuwa na miongozo inayotoa maelekezo kwa kila mdau, ikianisha majukumu na wajibu wake katika kufanikisha ulinzi huo kwa waandishi wa habari.

Soko anasema, mfumo unapaswa kuainisha namna wanahabari wanapaswa kuwajibika kazini pia wadau wengine wa habari wanavyopaswa kumhakikishia mwandishi wa habari kazini hakutwi na vikwazo na hasa visivyo vya kisheria.

> **"** Ni vema serikali ikaendelea kuwasikiliza wadau katika eneo hili kwa sababu waandishi wa habari ni kati ya wadau muhimu sana katika maendeleo ya nchi.

### KANZI DATA MUHIMU

"Kati ya mambo muhimu, mfumo unapaswa kuwa na kanzi data ya waandishi wote waliosajiliwa nchini. Pia, kanzi data hiyo iwe ina rekodi matukio yote yaliyohatarisha usalama wa waandishi wa habari wakati wakitekeleza majukumu yao, ili iwe rahisi kufanya ufuatiliaji wa matukio hayo na kufanya tathimini pale itakapohitajika," anafafanua Soko.

Pia, anataja wajibu wa kuwapo kamati jumuishi itakayokuwa ndio kiongozi wa utekelezaji yatakayokubaliwa ndani ya mfumo husikia . Analitaja hilo lina mhakikishia kila mdau kupata kilichokubaliwa na kamati, kwa maana ya wajibu na dhamana zao kwa usalama wa mwandishi wa habari.

"Wenzetu Kenya na nchi nyingine kadhaa za jirani, zina mifumo kama hii na inawasaidia kuhakikisha ulinzi wa waandishi wa habari.

"Ni vema na sisi tukawa na mfumo kama huu, ili kuhakikisha kuwa mchango wa sekta ya habari katika kusukuma mbele maendeleo ya nchi unaimarika," anasema Soko.

### DALILI YA KUBOREKA

Hata hivyo, Soko anakiri kwamba katika miaka michache ya karibuni, usalama kwa waandishi wa habari umeimarika, kulinganisha na nyuma

"Ni kweli bado yapo matukio yanayohatarisha usalama wa waandishi wanapo kuwa kazini, lakini wingi na uzito wa matukio hayo umepungua katika miaka ya hivi karibuni," anasema.

Soko anabainisha furaha kuona serikali inakaa na kuwasilikiliza wadau wa habari, jambo linalowezesha mambo kadhaa ikiwamo mabadiliko ya sheria zinazohusiana na masuala la habari.

Anasema, ingawa mabadiliko hayo hayajatoa hakikisho la ulinzi wa waandishi wa habari kwa kiasi kikubwa, lakini kupitia mabadiliko hayo ya sheria na vipengele vingi vya sheria vilivyokwaza kazi za uandishi wa habari nchini viMdau wa habari, James Marenga, anasema ndani ya mabadiliko, kuna mambo mengi yanayopaswa kurekebishwa kwenye sheria zilizopo, pia ili kuwahakikishia ulinzi wa waandishi wa habari kazini.

Anaendelea; "Ni vema serikali ikaendelea kuwasikiliza wadau katika eneo hili kwa sababu waandishi wa habari ni kati ya wadau muhimu sana katika maendeleo ya nchi."

Marenga anatoa mfano wa yanayokwaza kwenye sheria, ni suala analoliita 'uchochezi' kwamba ni shida kwa majukumu yao.

"Sheria iliyopo haitoi ufafanuzi wa kina wa hicho kinachoitwa 'uchochezi', badala yake kuna ufafanuzi wa nia ya kufanya uchochezi. Hiyo inawafanya waandishi wengi hasa wale wanaofanya habari za uchunguzi, kujikuta katika matatizo kwa kuelezwa kuwa wamevunja sheria hiyo," anafafanua.

### HATARI MTANDAONI

Miaka kadhaa iliyopita, usalama wa waandishi wa habari umeihusishwa na madhara ya kimwili, pamoja na uharibifu wa vifaa vyao vya kazi. Lakini, kutokana na mabadiliko ya teknolojia, hivi sasa masuala ya usalama wa waandishi yanahusisha pia na matumizi ya mitandao ya habari.

Anataja nafasi yake, kwa sababu intaneti imechukua nafasi kubwa sana katika suala la upashanaji habari. Hivi sasa, waandishi binafsi na vyombo karibu vyote vya habari vinategemea intaneti na mitandao kama moja ya nyenzo kubwa ya utendaji wao.

Analalamika waandishi wa habari, kama ilivyo wengine katika jamii, ni waathirika wa uhalifu mitandaoni ikijumuisha kunukuliwa kwa kazi zao bila idhini yao, ni sehemu ya changamoto kwa waandishi wengi wanapitia.

Miaka kadhaa iliyopita, waandishi wengi walikuwa waoga kuwasiliana kwa simu za mikononi, wakihofu kudukuliwa na kwa baadhi ya waliokuwa vyanzo vya habari, nao waliogopa kuzungumza na waandishi kupitia simu kwa hofu hiyohiyo ya kudukuliwa.

Ni hali anayoitaja kuchangia kuporomoka kwa viwango vya waandishi wa habari, hata kuna wakati mitandao ya kijamii ilitumika kusambaza taarifa za kashfa na uongo kuhusu vyombo vya habari na waandishi wa habari.

Inatajwa, kwamba ilihatarisha usalama wa waandishi wa habari, kwani lilikuwa na unasaba wa uchochezi lakini hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya waliofanya hivyo.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa masuala ya usalama mtandaoni, Maxence Mello, ni vema waandishi wa habari wakachukua hatua za kujifunza namna ya kujilinda wao wenyewe binafsi na kulinda kazi zao mtandaoni.

"Wakati watu wengi wakiangalia athari za usalama wa waandishi kwa kuangalia hatari zinazomkabili mtu kimwili na uharibifu wa vifaa, hali ya dunia kwa sasa imebadilika sana kiasi cha kuwa na hatari nyingi dhidi ya mwandishi mtandaoni kuliko ilivyo kwa hatari ya kudhuriwa kimwili," anasema Mello.

Kwa mujibu wa Mello, sehemu kubwa ya matukio ya uhalifu yanayoripotiwa katika vituo vya usalama nchini, yanahusisha ya mtandaoni.

Hapo mdau Mello anashauri kuwepo na mfumo unaohakikisha wanahabari wanalindwa dhidi ya uhalifu wa mtandaoni, kwani adha inayowakabili ni kukosekana habari za mitandao, ambayo ni njia muhimu duniani sasa.

"Iwapo waandishi wataingiwa na woga na kuacha kuchapisha maudhui yao mitandaoni kutokana na hofu, ipo hatari jamii ikakosa taarifa muhimu," anasema Mello.

AFYA

# Kikundi Daraja Salama kilivyofika Temeke kuchangia damu, daktari akiwazawadia somo

## • Waambiwa: Enyi mashujaa...haturejeshi majibu ya virusi

**Na Halfani Chusi**

NI huruma au kuguswa? Ndilo swali la kujiuliza kutokana na kikundi cha Daraja Salama ambacho maskani yake ni mkoani Dar es Salaam, kinapoamua kwa kujitolea bila ya kusukumwa na mtu yoyote kuchangia damu, ili kuokoa maisha ya wahitaji kutoka hospitalini.

Hapo, wakajumuika na wanafamilia zao kufika Hospitali ya Rufani Temeke, kwa ajili ya kuchangia damu. Wanafika na kupokelewa kwa bashasha na uongozi wa hospitali, ambao walitafsiri kama ni “mashujaa waliofika hapo kuokoa maisha ya wagonjwa hasa wahitaji wa damu.”

Nipashe iliyokuwa bega kwa bega, mara moja inabaini kuwa si mara ya kwanza kwao kutoa misaada ya kijamii na kwamba walishafanya hivyo kwa kuwatembelea watoto yatima na kutoa msaada kwa wagonjwa wasio na ndugu katika hospitali kadhaa nchini.

Ila kwa siku hiyo, hawakuwa na ajenda ya kuchangia damu pekee, pia walibeba vitu kadhaa kwa ajili wa kuwapatia wagonjwa mbalimbali wanaopatiwa matibabu hospitalini hapo, kwa lengo la kuwafariji. Kiongozi wa Kikundi cha Daraja Salama, Momack Komba, anasema wameamua kuchangia damu kwa kuwa si bidhaa inayoweza kupatikana mahali pengine, kinyume na mwili wa binadamu.

Kinadharia ya kijamii, kiafya na hata kiuchumi, kuna sababu zote kwa mtu mwenye afya njema na damu ya kutosha, kuwasaidia wengine ili kukoa maisha yao.

“Sisi Daraja Salama tunasema ‘furaha kwa wote’ na huwa tunafanya hivi sio kwa hospitali pekee, huwa tunatembelea yatima, wajane na wazee wasiojiweza. Kwa kiasi kikubwa,na imekuwa kama shughuli yetu ya kila siku.

“Hii ni mara yetu ya kwanza kuchangia damu, Mungu ametupa kibali, tumefikiria na tumeweza kufika hapa kwa ajili ya kuchangia damu, lakini tunafikiria kuendelea kufika kwenye maeneo mengine kuendelea kuchangia damu, kutokana na maelekezo ya wataalamu wa afya,” anafafanua.



Wana kikundi cha Daraja Salama, wakiwa kwenye foleni kuchangia damu, walipozuru kwenye Hospitali ya Rufani ya Temeke. **PICHA: HALFANI CHUSI**

Ni hoja inayoungwa mkono na Kiongozi wa Matukio Daraja Salama, Jenirosa Sinkala, anayesema, pia wamebeba vyakula, maji na matunda kwa ajili ya kuwapatia wagonjwa wasio na ndugu.

“Tumeleta pia pampasi kwa ajili ya watoto wadogo ambao wapo humu hospitali, ndugu zao hawajapatikana kirahisi, kuna juisi kwa ajili ya watoto na mahitaji mengine kwaajili ya kinamama wajawazito.

“Kuna watu huwa wanaletwa hapa, wamepata ajali wanahitaji damu ili kuokoa uhai wao, kwa hiyo kama jamii tunapaswa kujitoa kuchangia damu kwa nguvu zote, ili kuzuia vifo vitokanavyo na ukosefu wa damu,” anahimiza na kuendeleza hoja:

### OFISA AFYA AWAFUNDA

Ofisa Afya, Juhudi Nyambuka, anasema hospitali yao ipo karibu na Uwanja wa Taifa, kwamba ajali nyingi hutokea maeneo hayo na sehemu kuu ya kukimbilia ni kwenye hospitali yao, hivyo kuna muda huwa wanaelemewa na wagonjwa.

Anasifu kitendo cha kikundi hicho kujitolea kuchangia damu, kwao ni jambo kubwa na wanastahili kuungwa mkono, kwa kuwa wanachokifanya ni kwa ajili ya maisha ya Watanzania na umma kwa jumla.

Mtabibu huyo, ambaye muda wote hakusita kuonyesha furaha aliyoipata kutokana na ugeni huo ofisini kwake, anaendelea kueleza kuwa mtu yeyote anaweza kuchangia damu na kwamba milango yao ipo wazi siku zote kwa ajili ya hilo.

“Kutoa damu ni hiari ya mtu, hatuwezi kumfunga kamba, wala kumlazimisha kwa viboko. Wale ambao wanajitokeza kwa hiari sisi tunawashukuru sana na tunawarekodi, ili tuwajue kwamba ni wadau wetu muhimu” anasema daktari huyo

Anafafanua kuwa Kukosekana damu kuna hatarisha kifo na kwamba watoa huduma huwa wanaumia sana, kuona mgonjwa anapoteza maisha kwa kukosa damu, lakini hata hali ya wakati mwingine kuchelewa kutoa huduma kwa sababu ya kutafuta damu kwingineko.

“Sasa hivi kuna kitu kingine ambacho tunakifanya kwenye damu, tunaichakata kuna mazao ya damu mengine yanasaidia kuokoa wagonjwa, kwa sababu kuna mtu mwingine hahitaji, ila anahitaji chembe chembe hai nyeupe, ili aweze kupata ahuweni.

“Kwa sasa tuna mashine ambayo kazi yake ni kuchakata damu na kupata zile chembechembe kwa wale ambao watakuwa hawana shida ya kuongezwa damu,” anasema.

Daktari huyo anawatoa hofu wote wanaosita kwenda kuchangia damu kwa kuhofia kupimwa virusi vya Ukimwi, akiwapa ufafanuzi: “Upimaji wa virusi vya Ukimwi ni hiari ya mtu mwenyewe. Kwa hiyo niwatoe hofu wale wote wanaodhani ukija kupima hapa utapimwa na virusi vya Ukimwi, hapana!

Anasema atakayechangia damu pia atapata faida ya kujua maendeleo ya damu yake kwa sasa hivi, kwa sababu kupitia damu yake tunaweza kumtambua hata kama ana shida ya ini na akaanza kupata matibabu mapema.

### HALI BENKI YA DAMU

Nyambuka anasema, hospitalini Temeke kuna hitajika uniti 600 za damu kumudu hali ya wagonjwa wanaofika hapo kwa ajili ya matibabau, huku kiasi wanachoweza kukusanya na kuwa nacho stoo ni uniti 400 pekee; wana upungufu wa theluthi moja ya mahitaji.

> **Kwa sasa tuna mashine ambayo kazi yake ni kuchakata damu na kupata zile chembechembe kwa wale ambao watakuwa hawana shida ya kuongezwa damu.**

## Ushuhuda wa vita vya Dk. Samia kutanua ulingo wa mbolea nchini

**INATOKA UK.11**

matarajio ya kuzalisha tani 70,000 za mbolea katika mwaka wa fedha uliopo, matarajio ni kupatikana mbolea kwa wingi kitaifa.

Ruzuku ilianza katika mwaka wa fedha uliopita na serikali kupitia Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ikatangaza ruzuku ya Sh. bilioni 150 kwa ajili ya mbolea kwa wakulima nchini.

Kwa mujibu wa Waziri Bashe, utaratibu wa mbolea ya ruzuku inawekewa lebo maalumu, kuzitofautisha na zinazouzwa madukani.

Mara baada ya Rais Dk. Samia kuingia madarakani, mbali na kukaribisha uwekezaji wa viwanda, kulijengwa maabara ya huduma za mbolea nchini.

### MBOLEA INAVYOTUMIKA

Katika kutathmini matumizi ya mbolea kitaifa, TFRA ilibaini kuwapo matumzi hafifu ya mbolea mikoa ya Lindi na Mtwara, hata hatua zikachukuliwa kidhibiti kasoro hizo mwaka jana.

Mkurugenzi wa TFRA Dk. Stephan Ngailo, anasimulia walivyochukua jukumu wakishirikiana na uongozi wa mikoa hiyo wakihamasisha matumizi sahihi ya mbolea shambani, wakitenga maeneo maalumu, kupima afya ya udongo mashamba husika, kabla ya kutambua mbolea sahihi kwa maeneo hayo.

Dk. Ngailo anafafanua hatua zilizochukuliwa ikianza kwa kushirikiana na wakulima kupitia vikundi vyao, pia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Naliendele, Mtwara na wataalamu wa kilimo wa mikoa hiyo.

Hapo ikifuatia kuchukuliwa sampuli za udongo kupimwa katika Kituo cha Mlingano Tanga, mapungufu yaliyobainika yakaanza kufanyiwa utekelezaji kwa wakulima husika na mazao yao.

Ni mchakato ambao Dk. Ngailo, anaueleza ulitumia mbolea tani tano kwa mafanikio.

MAZINGIRA

# Operesheni ya kuhifadhi misitu kijijini inavyoipatia faida zahanati iliyotimia

• Jengo mama na mtoto, nyumba ya mganga...

**Na Beatrice Philemon,** aliyekuwa Namtumbo

HAIKUWA rahisi kwa wananchi kijijini Kitanda, kutembea umbali kilomita 80 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma, kupata jengo la kisasa la mama na mtoto na nyumba mbili za waganga, kutokana na shughuli za uhifadhi wa misitu kijijini kwao.

Kazi ya uhifadhi wa misitu kijijini Kitanda, ilianza mwaka 2016, baada ya halmashauri yao, Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Shirika la Uhifadhi na Maendeleo la Mpingo (MCDI) kuwatembelea na kufundisha wananchi uhifadhi bora wa misitu na uvunaji endelevu wa rasilimali zake.

Ni dhana inayowasaidia wananchi kuanzisha msitu wa hifadhi ya kijiji, unaowasaidia sasa kupata fedha inayofadhili miradi ya maendeleo kijijini, huku ikipunguza ukataji miti, maisha yao yakiboreka, wakikabiliana na maisha ya jamii na mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza na Nipashe, Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Katibu wa Ulinzi na Usalama Kijiji cha Kitanda, Neema Ng'oma anasema: "Tunajisikia raha sana kinamama katika kijiji hiki tumepata jengo zuri, ambalo litatusitiri wakati wa kujifungua, jengo lenye utulivu na nafasi ya kutosha.

"Hakuna usumbufu tena wakati wa kujifungua, wala kutembea kilomita 60 kwenda kujifungua katika Kituo cha Afya cha Aga au kilomita 80 katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo..."

Kabla ya mradi huo, anasema wajawazito kijijini hapo walitaabika wakati wa kujifungua, hawakuwa na sehemu tulivu ya kujifungua na hapakuwa rafiki kwao.

Neema anasema wagonjwa waliofika kutibiwa maradhi mengine katika zahanati ya kijijini hapo, hawakuwa na faragha, akitaja chumba kilichotengwa kwa wajawazito kujifungua, kilikuwa kidogo, huku kikihudumia idadi anayotaja kuwa ni watu watano.

"Tumefanikiwa kupata mafanikio haya kupitia mradi wa miaka mitano unaoitwa 'Leading The Change Project' unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA) kupitia Shirika la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori (WWF-Tanzania)," anasema.

Mradi huo ulikuwa unatekelezwa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Shirika la Uhifadhi na Maendeleo la Mpingo (MCDI) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo.



Jengo la Mama katika kijiji cha Kitanda, wilayani Namtumbo, linalotokana na mauzo ya magogo yaliyovunwa kutoka katika mradi wa kuhifadhi misitu kijijini hapo. P**ICHA: BEATRICE PHILEMON**

> **Tunashukuru MJUMITA, MCDI na Halmashauri ya wilaya ya Namtumbo kuleta mradi huu ambao umenufaisha zaidi ya wakazi 11,692 katika kijiji cha Kitanda.**

"Wananchi walifundishwa uhifadhi wa misitu na ukokotoaji wa magogo, elimu ya utawala bora, usimamizi wa fedha zinazotokana na biashara endelevu ya mazao ya misitu, utunzaji kumbukumbu na ubandikaji wa matangazo," anasema.

Pia, anafafanua darasa la namna ya kupata takwimu ya ujazo wa miti na gharama zake, uongozi bora, uandaaji taarifa za mauzo ya mazao misitu, utunzaji fedha, uwazi na kuitisha vikao vya kujulisha jamii mambo ya uhifadi misitu.

### SAUTI YA MWENYEKITI

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kitanda, Joseph Ng'onyani, anasema kupitia elimu waliyopata kutoka MJUMITA, MCDI na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, wametenga Msitu wa Hifadhi ya Kijiji unaoitwa 'Mtaungana' wenye hekta 11.930 kwa ajili ya usimamizi shirikishi.

"Kazi ya uhifadhi wa msitu ilianza rasmi mwaka 2016 katika kijiji chetu na ilipofika mwaka 2021 tulipata wavunaji wa mazao ya misitu, hata wakavuna magogo yenye mita za ujazo 369.362 (cubic meter) wakayauza kwa thamani Sh.107,115,000".

### MATUMIZI YA MAVUNO

Ngonyani anasema Sh.29,939,500 zilitumika kujenga jengo la kisasa la mama na mtoto kwenye zahanati; Sh.21,371,000 wakajenga nyumba mbili za waganga; Sh. milioni 2.7 zikatumika kununua pikipiki; moja kwa ajili ya wajumbe wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji kufanya doria msituni.

Zingine anataja ni shilingi milioni tatu zilitumika kununua madawati ya wanafunzi, Shule za Msingi Lugongoro, Kitanda na Mkomanile, ili kuwajengea wanafunzi mazingira bora ya kusoma na hata kuongeza ufaulu wao, pia wanafunzi hao wakibaki na somo la umuhimu wa kutunza misitu yao.

Katika mustakabali huo, hivi sasa viongozi wa vijiji wanapopanga bajeti, wanashirikisha pia walimu, lengo ni kutunua wigo shirikishi wa kutunza misitu.

"Elimu ya uhifadhi wa misitu imeleta mafanikio makubwa sana kwa wakazi wa kijiji chetu. Hivi sasa wananchi wanafuata sheria ya uhifadhi wa misitu. Kila kitu kinafanyika kwa uwazi na kushirikisha wananchi wakati wa kutekeleza miradi ya maendeleo ya kijiji, tofauti na miaka ya nyuma," anasema.

Pia, Ngonyani anaeleza ni kawaida yao, vikao vyote vinavyofanyika vinabandikwa kwenye mbao za matangazo katika ofisi ya serikali ya kijiji, kuwatanulia wananchi uelewa namna fedha zilizopatikana kutokana na uuzaji magogo na zinatumika kama akiba na matarajio katika matumizi.

"Tunashukuru MJUMITA, MCDI na Halmashauri ya wilaya ya Namtumbo kuleta mradi huu ambao umenufaisha zaidi ya wakazi 11,692 katika kijiji cha Kitanda ," anasema.

### OFISA MISITU NAMTUMBO

Gravas Mwalyombo ni Ofisa Misitu wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, anasema, "Tunashukuru kupata huu mradi, kwa sababu umepunguza gharama za halmashauri kusimamia misitu.

"Tunasaidiwa na kijiji cha Kitanda kuhifadhi na kusimamia msitu, sasa hivi wanapata taarifa kutoka kwa Mwenyekiti au Ofisa Mtendaji wa Kijiji kuhusu masuala yote ya uhifadhi na usimamizi wa misitu," anasema Mwalyombo, akisifu kipato chao wanakijiji kinawapa nafuu, sasa wanatumia fedha za serikali kugharamia mengine.

Pia, anasifu uelewa nao uko juu katika namna ya kuhifadhi misitu, kutunza kumbukumbu za kihasibu, pia fedha zao, ikiendana darasa la utawala bora, viongozi wa vijiji na wananchi kwa ujumla wanajua vyema kanuni za utoaji taarifa za fedha za kijiji.

Kwa mujibu wa Ngonyani, Kitanda ndicho kijiji pekee kimetengeza madawati ya shule kwa fedha za uhifadhi wa misitu kati ya vijiji 71 vya Halmashauri Namtumbo.

### WANAKIJIJI WANAVYOFUNGUKA

Saidi Komba, mwenye watoto 13 mkazi wa kijijini Kitanda, ana hoja: "Tumepata mafunzo ya uhifadhi wa misitu na kitu kilichomfurahisha zaidi kwenye mradi huu ni kupata jengo la mama na mtoto kupitia fedha za uhifadhi wa misitu."

Akizungumza kwa niaba ya wanawake wenzake, Stella Lwambano, anasema ingawa wamepata jengo la kisasa la mama na mtoto, wanaiomba serikali na wadau binafsi wawasaidie kupata vitanda vya kujifungua, pia kupatikane maji katika jengo hilo, kutawawezesha kuwa katika mazingira bora na salama zaidi.

Pia, kuna rai ya kuongezwa mganga mwingine, sasa yupo mmoja, hali kadhalika wapatiwe gari kusaidia mgonjwa anayezidiwa kumpeleka katika hospitali kubwa.

Modestus Komba, Mjumbe wa Kamati ya Maliasili, Msitu wa Hifadhi ya Kijiji, anasema kwenye mradi wao wa zahanati, sasa ina wagonjwa wengi, hivyo wanahitaji maboreso na huduma zaidi ya afya, huku akiomba zaidi elimu ya utawala bora na uhifadhi.,



# Wakulima wataka ujazo mbolea ya ruzuku kupunguzwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuzishawishi kampuni za uzalishaji mbolea hapa nchini kuweka kwenye ujazo kuanzia kilogramu mbili hadi tano ili kila mkulima apate mbolea ya ruzuku inayotolewa na serikali.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, mkulima wa mtama Sauda Mbeyu kutoka mkoani hapa alisema sio kila mkulima anauwezo wa kununua mfuko wa kilogramu 25, hivyo ujazo huo unasababisha wengine washindwe kupata mbolea.

Alisema serikali inapaswa kuliangalia hilo ili kila mkulima anunue mbolea hiyo na kuitumia shambani kwake kulingana na uwezo alionao.

Naye, Jackson Alexander alisema baadhi ya wakulima wanahitaji mbolea kiasi, hivyo anapokuta hakuna mfuko wa kilogramu tano anashindwa kununua.

Hata hivyo, Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Kanda ya Kati, Joshua Ng'ondya aliwahakikishia wananchi kuwa mbolea ya ujazo wa kilogramu tano ipo na kusisitiza wakulima kujisajili ili kupata mbolea hiyo.

Alisema wanapaswa kujisajili kwa mawakala ambao wanatambulika na serikali waliopatiwa mafunzo kwa ajili ya kutoa mbolea ya ruzuku.

Alibainisha kuwa mfumo wa utoaji mbolea umeboreshwa hivyo wakulima msimu huu wa kilimo watapata mbolea bila kikwazo chochote kutoka kwa wasambazaji.

# Ukifanya ununuzi nje ya mfumo faini mil.10/-

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imesema taasisi yoyote ya umma itakayofanya ununuzi nje ya Mfumo wa Ununuzi wa Umma (NeST) itatozwa faini ya kiasi kisichopungua Sh.milioni 10.

Akizungumza jana katika mafunzo wezeshi ya utumiaji wa mfumo huo jijini hapa, Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakim Maswi alisema kuanzishwa kwa mfumo huo wa kuendesha michakato ya zabuni za umma ni suala mtambuka na kwamba ni wajibu kwa taasisi zote za umma kujifunza mfumo ili kuutumia kwa usahihi.

"Napenda ieleweke kuwa serikali inaziwajibisha taasisi zake kutumia mfumo huu wa ununuzi, hivyo michakato yote ya kufanya ununuzi wa umma serikalini, ni lazima ifanyike kupitia mfumo wa NeST," alisema Maswi.

Maswi aliongeza kuwa endapo taasisi yoyote ya umma itafanya ununuzi nje ya mfumo itakumbana na adhabu ya kutozwa faini isiyopungua kiasi cha sh.milioni 10 kwani kwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria na taratibu za ununuzi wa umma.

"Lakini pia mtambue kuwa kwakuwa kuna ulazima kwetu sisi taasisi za umma kufanya ununuzi kupitia mfumo huu basi muelewe pia kuwa kuna adhabu itakayotolewa kwa kila taasisi ambayo itathubutu kufanya ununuzi nje ya mfumo wa NeST,". Alisema.

Alisisitiza kuwa mafunzo kwa ajili ya matumizi ya mfumo huo yanaendelea kutolewa kwa maofisa wa taasisi za umma katika mikoa mbalimbali nchini huku ikielezwa kuwa mpaka ifikapo Oktoba Mosi matumizi ya mfumo wa NeST kwa ajili ya kufanya ununuzi wa umma yataanza rasmi na hakutakuwa na shughuli yoyote ya ununuzi wa umma itakayofanyika nje ya NeST.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri wa Kilimo Hussen Bashe (wa pili kulia) na Waziri wa Mifugo Abdalla Ulega walipokua wakielekea kukagua gari aina ya FAW iliyotengenezwa nchini katika kiwanda cha GFA kilichopo Kibaha lenye mtambo maalumu wa kuchimbia Visima vikubwa kabla ya kukabidhi vifaa kwa ajili ya miradi mbali mbali kwa Wizara ya Kilimo kwenye maonyesho ya Nanenane jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waomba kuandikiwa maandiko miradi wapate mikopo benki

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKULIMA na wafugaji wa Kanda ya Kati wamekiomba Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kutoa elimu ya kuandika maandiko ya miradi yatakayosaidia kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha ili kuimarisha shughuli zao.

Mkulima wa Kijiji cha Dabalo wilayani Chamwino, Yohana Yoramu na Jeni Mazengo kutoka Kijiji cha Nagulo wilayani Bahi walitoa ombi hilo jana walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari kwenye banda ya maonesho la chuo hiyo kwenye Uwanja wa Nanenane Nzuguni.

Yoramu alisema kuna umuhimu wa wataalamu kutoa elimu ya uandikaji wa maandiko hayo ili kufanya shughuli zao kuwa na tija.

Alisema: "Chuo cha Mipango ni chuo kinachozalisha wataalamu mbalimbali wakiwemo watafiti wa miradi, hivyo sisi wakulima na wafugaji tunaomba tupewe elimu na tuandikiwe maandiko ili tuombe kwenye taasisi za kifedha ambazo zitakazotuwezesha kuinua ufugaji na ukulima wetu ambao wengi wao bado wanalima na kufunga kienyeji bila utaalamu," alisema.

Naye, Jeni alisema kuwa wafugaji na wakulima wamelazimika kuomba elimu hiyo kwa kuwa wengi wao hawana uelewa wa kuandika miradi. Akizungumza na wakulima na wafugaji hao, Mhadhiri wa Chuo hicho, Dk.Maclean Mwamlangala, alisema wamekuwa wakishirikiana na wajasiriamali, wakulima, wavuvi na wafugaji katika kuwaandikia maandiko ya kuwawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha.

Alisema chuo hicho kimekuwa kikisaidia katika kuwaelimisha wakulima, wavuvi na wafugaji namna ya kuboresha sekta zao kwa kupitia wataalam na jinsi ya kupata mikopo itakayobadilisha maisha yao.

# Hospitali ya Dodoma ya kwanza duniani kutibu waliovunjika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, imekuwa ya kwanza duniani katika kutoa huduma za kutibu wagonjwa waliopata ajali na kuvunjika mifupa.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk.Ernest Ibenzi alibainisha hayo jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utoaji wa huduma na mwelekeo wa mwaka 2023/24.

Alisema wamekuwa wakitumia teknolojia kwenye magonjwa ya mifupa ambayo inasaidia mgonjwa kupona haraka na kuendelea na shughuli zake.

"Utafiti ulifanywa na mtandao wa watalaamu ambao wamejikita kutengeneza vifaa tiba vya watu wanaovunjika, wana vituo zaidi ya 300 duniani na hapa nchini wapo Hospitali ya Dodoma, kwa siku tunahudumia wagonjwa 10."

"Kulingana na sifa walizokuwa wameweka waliona hospitali yetu ni ya kwanza kidunia, ikiwamo kupona kwa muda mfupi na kurejea kwenye majukumu yao,"alisema.

Alieleza kuwa kutokana na kupiga hatua ya matibabu hayo kwasasa wataalamu wanazunguka hospitali zingine kuwapatia vifaa na kutibu.

"Tumefika Hospitali ya Mount Meru, Shinyanga, Njombe na tunatarajia kwenda Morogoro na hata maeneo ambayo hatujafika tunawapigia simu wenzetu kuuliza wapi pana wagonjwa wengi wa mifupa iliyovunjika wameshindwa kutembea tuje kuwasaidia watembee haraka na kurudi kwenye majukumu yao,"alisema.

Alisema maendeleo ya sayansi na teknolojia ndio yamechangia utoaji huduma hiyo.

Alisema kuna wagonjwa wa miguu ambao wametibiwa kwa njia hiyo wamerejea kwenye majukumu yao ndani ya wiki moja na wale waliovunjika mkono wao ni ndani ya siku moja anaweza kufanya shughuli zake.

Kadhalika, alisema hospitali imewekeza kwenye hewa tiba ili kuondokana na tatizo lililojitokeza wakati wa janga la ugonjwa wa corona la kufuata hewa hiyo mkoani Arusha.

"Hospitali yetu kuna kisima cha hewa tiba, kinafungulia kama bomba la maji mgonjwa anapata ya kutosha kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali,"alisema.

Alisema vitanda 297 vimeunganishwa na hewa tiba. Kuhusu wodi ya watoto kulazimika kulala wawili, alisema ndani ya wiki mbili jengo jipya litaanza kitumika na kuondokana na tatizo hilo.





# UDSM yaibuka kinara wa ubunifu maonyesho Nanenane

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeibuka kidedea katika kundi la taasisi za elimu baada ya kubuni teknolojia ya kumwongezea thamani mdudu senene kwa kutumia mafuta yake kutengeneza vyakula vinavyosaidia kuepuka magonjwa ya afya ya moyo.

UDSM imepata ushindi huo kwenye hitimisho la maonesho ya kimataifa ya wakulima, wafugaji na wavuvi yaliyofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, kushirikisha nchi za jirani. Akizungumza na waandishi wa habari, Mkufunzi Msaidizi kutoka Idara ya Sayansi ya Chakula na Teknolojia ya UDSM, Crispin Ndelende alisema mafuta ya senene imebainika kusaidia kuepuka magonjwa ya kiharusi na shinikizo la damu pamoja na kuimarisha afya ya ubongo.

Alisema senene ni mdudu ambaye ana protini kwa wingi, anayo mafuta yenye afya yanayofahamika kama omega3 na omega6 na yamekuwa yakisaidia afya ya moyo na kujenga afya ya ubongo kwa mtoto na kwa mtu mzima kuweza kuweka sawa kumbukumbu.

"Lakini senene ana sifa nyingi kuwa na madini chuma, zinki pamoja na vitamin B12 ambavyo vyote kwa pamoja ni muhimu kwa afya ya binadamu," alisema Ndelende.

Alisema kutokana na watu kupata changamoto ya kula mdudu senene kwa ajili ya kutatua changamoto za kiafya, UDSM wamekuja na teknolojia ya kutengeneza bidhaa mbalimbali za vyakula ambapo ndani yake kuna virutubisho vya senene.

"Kama idara tuliweza kupata senene tukawachakata na baada ya kukamua mafuta ya senene na kubaki na makapi ambayo yameweza kutengeneza bidhaa mbalimbali ikiwamo na mkate, biskuti na vyakula mbalimbali ili mtu akishindwa kula senene ale bidhaa hizo," alisema Ndelende.

Naye Mkurugenzi wa Shahada za Awali, Kampasi ya (DUCE), Dk. Herzon Onditi, alisema katika maonesho hayo wamekuja na vitu mbalimbali vilivyoibuliwa na wanataaluma kwa ajili ya kuzisambaza ziweze kutumika kwa wananchi pamoja na wakulima.

Alisema katika maonyesho hayo wamekuja na ubunifu wa mashine mbalimbali ikiwemo ya kuwasaidia wakulima kukausha korosho na kuongeza thamani, mitambo ya kusaga vyakula mbalimbali vya kusaidia wajasiriamali wadogo pamoja na teknolojia za ufugaji wa samaki.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Tigo, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Abbas Abdulrahman (kushoto), kuhusu kampuni hiyo inavyoshirikiana na serikali katika kuboresha mifumo ya malipo kwa wakulima kupitia Tigo Pesa na huduma mbalimbali, alipotembelea maonyesho ya wakulima Nanenane jijini Mbeya juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# IAA yatenga mil.100/- kuwawezesha wahitimu

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

CHUO cha Uhasibu Arusha (IAA) kimetenga Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuwawezesha wahitimu wenye mawazo bora ya kibiashara ili kuwawezesha kutimiza malengo yao.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa chuo hicho, Profesa Eliamani Sedoyeka kwenye maeneo ya wakulima nane nane ya kimataifa yanayoendelea jijini Mbeya.

Alisema wameamua kutenga fedha hizo ikiwa ni jitahada za kutambua mchango wa vijana katika kutimiza malengo yao ikiwemo uanzishwaji wa kampuni na kusajili biashara zao.

"Ni sehemu ya ubunifu katika kuhakikisha chuo chetu kinatambua mchango wa vijana ambao wanabuni vitu mbalimbali. Mbali na kutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia kufanikisha mawazo yao lakini pia kila mwaka tunaandaa wiki ya maonesho ya ubunifu ambao tunatoa nafasi kwa vijana kuonesha mambo waliyonayo na kuwasaidia kuboresha vitu wanavyovitengeneza ushauri wa kitaalam na kuwaunganisha na wadau ili kukuza mawazo yao au ubunifu na kupata fursa," alisema Prof. Sedoyeka.

Aliongeza kuwa mbali na kuwaandaa vijana kuwa wabunifu wenye uwezo wa kukabiliana na soko la ajira lakini pia chuo kinaendelea kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vitendo, kuandaa mawazo ya biashara ili kuwasaidia kujikwamua kiuchumi badala ya kutegemea kozi pekee wanazozisoma.

# Bil.8/- kujenga miundombinu ya umwagiliaji vituo 17

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

SHILINGI bilioni nane zimetengwa kwa ajili ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika vituo 17 vya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI). Akizungumzia mikakati ya kuboresha utafiti wa mbegu bora za mazao mbalimbali katika maonesho ya wakulima, wafugaji na wavuvi yanayofanyika jijini Mbeya, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk Geofrey Mkamilo, alisema tayari mchakato kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo umeshaanza.

Dk. Mkamilo alisema fedha hizo zitatumika kujenga miundombinu hiyo katika hekta 854 ambako ni kwenye vituo vyote vya utafiti nchini ili kuimarisha mifumo ya umwagiliaji wakati wa uzalishaji wa mbegu.

Alisema mpaka sasa ujenzi huo umeanza kwa maana ya kwamba ameshapatikana mkandarasi anayejulikana kama Pro Agro Global Limited, mikataba imesha-sainiwa mwaka wa fedha uliopita na muda wowote atanza ujenzi huo katika vituo hivyo 17.

"Tayari mkandarasi aliyepewa kazi hiyo ameshatengeneza ramani, kuna sehemu anachimba mabwawa na kujenga matangi ya maji. Kazi ya usanifu imeshaanza kwenye vituo vyote katika mwaka huu wa fedha ulioanza Julai kuna bajeti ya shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuendelea na ujenzi." Alisema Dk. Mkamilo.

Alisema jukumu la taasisi hiyo lilivyo la kutafiti, kusimamia, kuhamasisha na kuratibu shughuli za utafiti nchini, kupitia miundombinu hiyo ya umwagiliaji itaongeza tija katika uzalishaji wa mbegu bora katika kipindi kifupi.

Alitaja vituo vinavyojengwa miundombinu hiyo ya umwagiliaji kuwa ni TARI Maruku kilichoko Bukoba, Ukiliguru Mwanza, Tumbi Tabora, Kihinga Kigoma na Uyole Mbeya.

Vituo vingine ni Kifyulilo Iringa, Naliendele Mtwara, Kibaha Pwani, Mikocheni Dar es Salaam, Dakawa – Mvomero, Ifakara Kilombero, Ilonga Morogoro na Hombolo Dodoma.

Vingine ni Makutupora Dodoma, Mlingano Tanga, Tengeru Arusha na Selian Arusha.

Naye Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe, alimweleza Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango kuwa mwaka huu tayari ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji imeanza ili utafiti uweze kuendelea kwa mwaka mzima.





# Kamishna wa Polisi ahimiza uadilifu, haki, ushirikiano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad amewataka wakaguzi wa polisi wa shehia, kufanya kazi kwa uadilifu na kutenda haki ili kudumisha ushirikiano baina yao na jamii.

Amesema hatua hiyo itawawezesha wananchi kuliamini jeshi hilo na kufichua matukio ya kihalifu na wahalifu yanayotokea katika jamii.

Aliyasema hayo jana katika ukumbi wa mikutano wa Polisi visiwani hapa wakati akifungua mafunzo ya Polisi Jamii yanayolenga kuwajengea uwezo wakaguzi ambao wanahudumu katika shehia kwa lengo la kudumisha ushirikiano baina ya Jeshi la Polisi na jamii.

Alisema wakaguzi ni nguzo muhimu katika kuunganisha wananchi na Jeshi la Polisi, hivyo utekelezaji wa majukumu yao unapaswa kuzingatia maadili na taratibu za kisheria ili kuendelea kuleta heshima ya jeshi hilo.

"Napenda kusisitiza kutambua umuhimu wa jukumu ambalo kila mmoja wenu analo kama ofisa wa Polisi jamii.

Mtambue kuwa nyinyi ni nyuso za matumaini, huruma na mabadiliko chanya kwenye shehia zenu, hivyo kujitolea kwenu kuhudumu kwa uadilifu na huruma kutakuwa chachu ya kujenga madaraja kati ya Jeshi la Polisi na watu mnaowahudumia" alisema Kamishna Hamad.

Aidha, alisema wakaguzi shehia ni kama washauri wa masuala ya kiusalama katika ngazi ya shehia hivyo wanapaswa kubaini vyanzo vya matukio ya kihalifu na kutafuta mbinu zitakazosaidia kutatua changamoto hizo katika shehia zao.

"Polisi jamii inazingatia kuzuia uhalifu kabla haujatokea kuliko mbinu ya kupambana na uhalifu, jambo ambalo linatumia gharama kubwa" alisema.

Hivyo, aliwataka wakaguzi hao kufanya mikutano mbalimbali katika shehia zao kutoa elimu ambayo itasaidia wananchi kutambua dhana ya Polisi Jamii kuwa ni nyenzo muhimu inayowakaribisha wananchi na Jeshi katika kuzuia uhalifu.

Naye Mratibu wa Polisi, Dk. Ezekiele Kyogo kutoka Kamisheni ya Polisi Jamii,Kitengo cha Ushirikishwaji wa Jamii Makao Makuu ya Polisi Dodoma, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wakaguzi shehia katika kutekeleza majukumu yao ili dhamira ya Jeshi la Polisi katika kushirikiana na jamii kutimia.

Hivyo aliwataka wakaguzi hao kutumia mafunzo hayo kama sehemu ya kuboresha utendaji wao katika shehia wanazohudumu kwa kuwa utendaji bora ndiyo msingi wa kuaminiwa na jamii.

Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Veronica Fubule, alisema shirika hilo limefadhili mafunzo hayo ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za kuimarisha usalama na amani ili kufikia maendeleo ya nchi.

Alisema: "Nchi bila amani hakuna maendeleo, hivyo uwepo wa amani ndio msingi wa maendeleo kwa nchi yeyote ulimwenguni".



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla akimtwisha ndoo ya maji, Fatma Khamis Khamis mkazi wa Wandaras ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa kisima cha maji safi na salama kilichojengwa kwa fedha za Mbunge wa Jimbo la Magomeni, Zanzibar juzi. **PICHA: OMPRZ**

# Bei za mafuta ya petroli, dizeli zaongezeka Zanzibar

**Na Rahma Suleima,**
ZANZIBAR

BEI ya mafuta ya petroli visiwani Zanzibar katika kipindi cha Agosti imepanda ikilinganishwa na Julai.

Kwa mwezi huu nishati hiyo kwa lita moja inauzwa shilingi 2,970 kutoka shilingi 2,700 ya mwezi wa Julai likiwa ni ongezeko la shilingi 270 sawa na asilimia 10.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari ofisini kwake jana Mjini Zanzibar, Meneja Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mbaraka Hassan Haji, alisema pia bei ya mafuta ya dizeli na mafuta ya ndege imeongezeka.

Alisema bei ya dizeli kwa Julai ilikuwa shilingi 2,746, kwa mwezi huu itauzwa kwa shilingi 2,843 ambayo imeongezeka kwa shilingi 97 sawa na asilimia nne.

Mbarouk alisema mafuta ya ndege yalikuwa yanauzwa kwa Sh. 2,190 katika kipindi cha mwezi uliopita na sasa yatauzwa kwa shilingi 2,365 ikiwa ni ongezeko la asilimia 175 sawa na asilimia nane, huku maafuta ya taa yamebakia bei yake ya kawaida ya shilingi 2,921.

Alisema mabadiliko ya kupanda kwa bei hizo imesababishwa na kubadilika kwa gharama za mafuta katika soko la dunia na utofauti wa dola na shilingi.

Alisema ZURA inapanga bei kwa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwemo kubadilika kwa wastani wa bei za uuzaji wa bidhaa hizo katika soko la dunia pamoja na soko la ndani kupitia Bandari ya Dar es salam.

Alisema pia ZURA inapanga bei kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani kwa mwezi uliopita ili kupata kianzio cha kufanyika mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi huu.

Mbarouk alisema pia ZURA huangalia gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es salam, kuangalia thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Marekani, gharama za usafiri, kodi za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Aidha, alisema mamalaka hiyo, haitasita kuwachukulia hatua za kisheria na kanuni kwa wamiliki wa vituo vya mafuta wanaozuia mafuta kutoyauza kwa kisingizio cha kuwatia hofu wananchi.

# Mjumbe H'shauri Kuu CCM akunwa utekelezaji ilani

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, amesema ilani ya Chama Cha Mapinduzi imetekelezwa vyema katika majimbo yote.

Amesema hatua hiyo inaweka wazi ushindi wa CCM katika ngazi zote katika uchaguzi wa mkuu wa mwaka 2025.

Hemed aliyasema hayo wakati akizungumza na wanachama wa CCM katika majimbo ya Amani, Shauri Moyo na Kwahani ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya kukagua uhai wa chama Mkoa wa Mjini Unguja Kichama.

Alisema miradi mikubwa imetekelezwa chini ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa lengo la kuinua hali za wananchi kama ambavyo ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 inavyoelekeza hivyo.

Mjumbe huyo ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, alikemea vitendo vya usaliti na makundi ndani ya CCM akisema hayana tija bali yanazorotesha utekelezaji wa ilani na mpango mkakati wa chama hicho kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Aidha, alisema kuwa CCM inaendeshwa kwa kusimamia katiba na kanuni hivyo, changamoto yoyote ndani ya chama itatuliwe kwa mujibu wa taratibu zilizopangwa ili haki na usawa utendeke kwa wanachama wote.

Mjumbe huyo alisisitiza nidhamu na uwajibikaji ndani ya chama kwa kuwataka viongozi kuwajibika katika kutekeleza ilani ya chama na kuwatumikia wananchi kwa kutekeleza ahadi zao walizoziahidi wakati wanaomba ridhaa ya kukaa madarakani mwaka 2020.

Alisema ushirikiano na uwajibikaji ndio silaha kubwa ya kuwapigia wapinzani, hivyo hakuna haja ya kuwagawa wanachama kwa maslahi binafsi na badala yake wawaunganishe wanachama kwa maslahi ya CCM na Taifa.

Mjumbe huyo wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa aliwataka vijana kukilinda, kukitumikia na kukitetea chama ambacho kina dhamira thabiti ya kusimamia maslahi yao na kuwataka kutumia fursa mbalimbali zilizopo nchini.

Hata hivyo, alisema serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itazijenga barabara zote za ndani kwa kiwango cha lami katika majimbo hayo ambazo zitachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza uchumi wa Zanzibar.

Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Ussi Salum Pondeza na Abdallah Manzi walisema kuwa ziara ya mjumbe huyo imefanyika muda sahihi baada ya kuwepo kwa makundi kipindi cha uchaguzi wa chama mwaka 2022.

Walisema kuwa CCM Mkoa wa Mjini kitasimamia umoja na mshikamano katika majimbo ili kuheshimu maono ya waasisi na viongozi wakuu wa chama hicho.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, Dogo Iddi Mabrouk, alisema kuwa jumuiya hiyo imepewa jukumu la malezi katika chama hivyo watahakikisha ifikapo uchaguzi wa mkuu wa mwaka 2025 majimbo yote yatakuwa chini ya CCM pamoja na kura nyingi kwa marais wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Magistrates Court (Approved Forms for the Primary Court)
GN. NO.943 (Contd)
FOMU MADAI-3

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya BUKOBA**
**Kituo cha KARABAGAINE Mkoa wa KAGERA**
**Shauri la Madai NO. 13/2022**
**Jina la mdai BENEZETH SEVELIAN KAMKURU**
**Jina la Mdaiwa TUMSIFU POSTA KYANDO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu za madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA: TUMSIFU POSTA KYANDO**
**KWAMBA:** Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 21 Mwezi AUGUST Mwaka 2023 ili kueleza kwa nini Hukumu isitekelezwe dhidi yako.
Kama hautahudhuria siku hiyo mahakama inaweza kusikiliza maombi haya bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 07 Mwezi AUGUST Mwaka 2023.

.....................................
**HAKIMU MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO KARABAGAINE**
**BUKOBA**

## KUPOTEA KWA CHETI



**UPENDO LUCAS KALANGURA** Anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo (Diploma)-kilicho tolewa na chuo cha Rungemba community Development Training Institute chenye namba za usajili **RU/DCD/009/1988,** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi **MOR/MOR/RB/254592/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**ELISHA JEREMIAH ISSANJA** anatangaza kupotea kwa kadi za magari zenye usajili namba **: T 659 AKW, T 746 ANT, T 463 ABP na T 346 DKY.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA :
**ARU/ARU/RB/257965/2023**

## KUPOTELEWA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA

**JULIUS CLEMENT NUMBI** ambaye ni msimamizi wa mirathi ya marehemu Clement Numbi Anatangaza kupotelewa na Nyaraka ya Umiliki wa kiwanja namba 9 kitalu"Y" kilichopo Ibinzamata Manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Julius kwa simu namba **0754-049692.**
Taarifa ya **Polisi:SHI/SHI/RB/259538/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**KILASARA JOHN CHRISTIAN** anatangaza kupotea kwa kadi ya **TREKTA** yenye usajili namba: **T 118 CDZ,** CHASSIS NAMBA: **PY550JE003363** na ENGINE NAMBA: **PYJ029T178757.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**dar/ost/rb/247529/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **KWICHIRIZA BENON TAREMWA** amepoteza kadi ya pikipiki yenye namba **MC168CDC** akiwa safarini.Taarifa za kupotea kwa kadi hiyo zimetotewa katika kituo cha Polisi na kupewa RB namba **KAG/KYA/RB/393636/2021** katika kituo cha Polisi Kyaka.Atakayeiona anaombwa kutoa taarifa katika kituo chochote cha Polisi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya........SENGEREMA**
**Kituo cha NYEHUNGE...Mkoa MWANZA**
**Shauri la Madai Na 62 NO 23**
**Jina la Madai OSCAR MAJIMA NA FRED GIRIAD**
**Jina la Mdaiwa ISAYA MASANJA FRED**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakamaza Mwanzo)**
**Kwa ISAYA MASANJA FRED WA NYEHUNGE (W) SENGEREMA – MWANZA SIMU NO: 0757741550**
**Kwa kuwa mdai/Wadai ameleta / wameleta madai yake / yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai)**

**PESA TSH .500,000/= ZA MAGUNIA MPUNGA** kwa hiyo inatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 11 Mwezi 08 Mwaka 2023 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi / msahidi wako na vielelezo vyote vinavyo husu shauri hili kw aajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hauto hudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya Wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 07 Mwezi 08 Mwaka 2023

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
NYEHUNGE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PAUL BENJAMIN NDUNGURU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA VITZ** yenye usajili namba: **T656 DYK,** CHASSIS NAMBA: **SCP900004979** na ENGINE NAMBA: **2SZ004991.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DAR/URA/RB/266379/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAID MAALIM MSUYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **KING LION** yenye usajili namba: **MC 181 ACA,** CHASSIS NAMBA: **LTBPJ8BG3E2K01341** na ENGINE NAMBA: **KL157FMI14J01650.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/188930/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SIRIYAKO HYAZINDI CHALE **anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T281AAJ aina ya HIACE. Chassis No. 71V6001178. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
Taarifa ya Polisi:
DOD/DOD/RB/266932/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

MURTAZA RUGEMALILA ZUBAILY anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA SOARER yenye usajili namba T437 DUN na CHASSI NAMBA: UZZ400009891. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
JB/292/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MWITA VICTOR NYAKIRIG** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LAND CRUISER** lenye jina la umiliki **TOP GUIDES SAFARIS LIMITED** yenye usajili namba: **T 238 CRY.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/266649/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na. 1050/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU AMINA ABDALLAH**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HAMIS .H. KAVIRA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 mwezi 08 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 07 mwaka 2023**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wakulima, wafugaji wakopeshwa tril. 3.9/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** MBEYA

WAKULIMA na wafugaji nchini wamenufaika na mikopo iliyotolewa na Benki ya CRDB ambayo katika kipindi cha msimu mitano hadi Julai mwaka huu, imetoa mikopo ya jumla ya Sh. trilioni 3.9.

Mkuu wa Kitengo cha Kilimo Biashara wa CRDB, Maregesi Shaaban, alibainisha hayo juzi alipomweleza Rais Samia Suluhu Hassan juzi alipotembelea banda la benki hiyo katika Maonesho ya Nanenane jijini Mbeya.

Alibainisha kuwa mwaka 2022, benki hiyo ilikuwa ya kwanza nchini kushusha riba za mikopo ya kilimo kufikia tarakimu moja, wakishusha kutoka asilimia 20 hadi asilimia tisa.

"Na katika mwaka huo huo, benki yetu ya CRDB ilichangia asilimia 43 kwenye mikopo yote itolewayo kwenye sekta ya kilimo nchini. Kati ya Sh. trilioni 2.299 zilizoelekezwa katika sekta hii, Benki ya CRDB ilitoa Sh. bilioni 998.081.

"Na kwa miezi sita ya kwanza mwaka huu, tayari tumekopesha zaidi ya Sh. trilioni 1.3, sehemu kubwa ikielekezwa katika kilimo cha mazao ya biashara na chakula, uvuvi, mifugo, uzalishaji wa malighafi za viwanda, ujenzi wa viwanda kwa ajili ya uchakataji mazao ya kilimo na mifugo, utengenezaji wa pembejeo, uendelezaji wa mazao ya misitu na biashara yake," alisema.

Ofisa huyo alisema kuwa kupitia taasisi yao ya CRDB Bank Foundation, wameanzisha programu ya uwezeshaji kwa vijana na wanawake ambapo kupitia programu hiyo iliyopewa jina la Imbeju, wanatoa mafunzo na mitaji wezeshi kwa vijana na wanawake ili wakuze miradi yao ya biashara na sekta ya kilimo ni moja kati ya vipaumbele vyao.

Alifafanua kuwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita hadi Juni 2023, jumla ya mikopo ya kilimo waliyoitoa ni zaidi ya Sh. trilioni 3.8. Kati ya mikopo hiyo, Sh. bilioni 495 zimeelekezwa kwenye mazao ya kimkakati kwa kuviwezesha vyama vya ushirika (AMCOS) 472 vyenye maelfu ya wanachama.

"Vilevile, benki yetu pia inashiriki kufufua ushirika kwa kuviongezea vyama na benki za ushirika mtaji. Jumla ya Sh. bilioni 10.2 zimetolewa huku Tandahimba Cooperative Bank (TACOBA) ikipata Sh. bilioni 3.2 na Sh. bilioni saba zimetolewa kwa Kilimanjaro Cooperative Bank Limited (KCBL).

"Katika msimu wa mwaka 2022/23, Benki ya CRDB imekopesha jumla ya Sh. bilioni 494.4 kwa AMCOS 472 zenye wanachama 751,080 nchini kote. Kati yake, benki imekopesha Sh. bilioni 250.5 kwa kampuni tano na AMCOS 30 zenye wakulima 6,000 katika maeneo ya Mtibwa, Kagera na Kilombero huku wakulima 375,000 wanaolima pamba katika halmashauri za Urambo, Mpanda, Chunya, Kahama na Kigoma ambao ni wanachama wa AMCOS 192 wakinufaika na jumla ya Sh. bilioni 75," alisema.

Alimwambia Rais Samia kuwa uwezeshaji wao haujaishia Tanzania Bara pekee, bali wamekuwa wanashirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwawezesha wajasiriamali wa awali, wa kati na wakubwa walioko Unguja na Pemba kupitia mpango maalum wa INUKA na UCHUMI WA BULUU kwa kutoa mikopo ili waongeze mitaji yao katika shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji, viwanda na biashara.

Alibainisha kuwa kupitia mpango huo, zaidi ya Sh. bilioni 60 zinaendelea kutolewa kwa wanufaika wasiopungua 50,000 walioko Zanzibar ili waongeze mitaji ya miradi yao na kuongeza tija kiuchumi.

"Ninakuhakikishia kuwa Benki ya CRDB itaendelea kushirikiana na serikali kuimarisha uchumi wa nchi kupitia sekta ya kilimo, hivyo nitumie fursa hii kuwakaribisha wakulima, wavuvi na wafugaji pamoja na wengine wote katika matawi yetu 257 yaliyopo Tanzania Bara na Zanzibari li tuwape suluhisho la mahitaji ya kukuza kilimo chao," alisema

Ofisa huyo wa CRDB pia alisema benki yao inashiriki kutoa mafunzo katika vituo atamizi chini ya mpango maalum wa BBT kupitia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Baadhi ya wakulima walioshiriki maonesho hayo, walisema benki hiyo imekuwa mkombozi kwao na kuleta mapinduzi katika kilimo kutokana na kuwapatia mikopo ya fedha na zana za kilimo.

Mkulima Halima Ally kutoka wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, alitoa ushuhuda mbele ya Rais Samia alivyonufaika na benki hiyo.

Rais Samia alipongeza Benki ya CRDB kwa kuwakopesha wakulima kwa riba nafuu ya asilimia tisa, akiitaka kuendelea kuwakopesha zana za kilimo na kufanya ufuatiliaji ili zana hizo zinapoharibika zitengenezwe badala ya kuzitelekeza.

## PSSSF yajivunia ushiriki wa vijana katika kilimo

**Na Khalfan Said,** MBEYA

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba, amesema uwekezaji uliofanywa na mfuko katika viwanda vya kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo utaongeza nguvu kwa wazo la Rais Samia Suluhu Hassan kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo chini ya Mpango wa BBT.

Kashimba ameyasema hayo juzi katika banda lao kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Tanzania katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya Agosti 7, 2023. Mfuko unatoa huduma kwa wanachama na wastaafu wa mfuko huo, pia elimu kuhusu fursa mbalimbali zilizopo, ukiwamo uwekezaji.

Alisema PSSSF tayari imewekeza katika kiwanda cha kuchakata tangawizi kilichoko Mamba Miamba, wilayani Same, Kiwanda cha Chai Mponde kilichoko wilayani Lushoto. Pia ina viwanda vya kuongeza thamani bidhaa za mifugo kama vile machinjio ya kisasa Nguru wilayani Mvomero na kiwanda cha bidhaa za ngozi mkoani Kilimanjaro.

Mradi wa Building wa Better Tomorrow (BBT) unaolenga kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo, maeneo ya mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko ulizinduliwa Agosti mwaka jana na tayari kundi la kwanza la vijana wapatao 800 wamehitimu mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuendesha kilimo biashara.




Rais Samia Suluhu Hassan (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo katika kilele cha maadhimisho ya wakulima Nanenane jijini Mbeya juzi. Katikati ni Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Teknolojia kuongeza thamani senene 'yafunika'

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

TEKNOLOJIA za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ikiwamo kumwongezea thamani senene kwa kutumia mafuta yake kutengeneza vyakula vinavyosaidia kuepuka magonjwa ya moyo, zimekipa chuo hicho ushindi wa kwanza kitaifa katika Maonesho ya Nanenane mwaka huu kwa kundi la taasisi za elimu.

UDSM ilipata ushindi huo katika hitimisho la maonesho hayo juzi kwenye viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya, yaliyoshirikisha pia nchi jirani.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkufunzi Msaidizi kutoka Idara ya Sayansi ya Chakula na Teknolojia UDSM, Crispin Ndelende, alisema mafuta ya senene yamebainika kusaidia kuepusha magonjwa ya kiharusi, shinikizo la damu na kuimarisha afya ya ubongo.

Alisema senene ana protini nyingi, ana mafuta yanayofahamika kama Omega3 na Omega6 yanayosaidia afya ya moyo na kujenga afya ya ubongo kwa mtoto na kwa mtu mzima kuwa na kumbukumbu.

"Lakini pia senene ana sifa nyingi kuwa na madini chuma, zinki pamoja na vitamin B12 ambavyo vyote kwa pamoja ni muhimu kwa afya ya binadamu," alisema Ndelende.

Alisema kuwa kutokana na watu kupata changamoto ya kula senene kwa ajili ya kutatua changamoto za kiafya, UDSM wamekuja na teknolojia ya kutengeneza bidhaa mbalimbali za vyakula ambavyo vitakuwa na virutubisho vya senene.

"Kama idara, tulipata senene, tukawachakata na baada ya kukamua mafuta ya senene na kubaki na makapi ambayo yameweza kutengeneza bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na mkate, biskuti na vyakula mbalimbali ili mtu akishindwa kula senene ale bidhaa hizo," alisema Ndelende.

Mkurugenzi wa Shahada za Awali Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu (DUCE), Dk. Herzon Onditi, alisema kuwa katika maonesho hayo wamekuja na vitu mbalimbali vilivyoibuliwa na wanataaluma kwa ajili ya kuzisambaza zitumike kwa wananchi na wakulima.

Alisema katika maonesho hayo wamekuja na ubunifu wa mashine mbalimbali ikiwamo ya kuwasaidia wakulima kukausha korosho na kuongeza thamani, mitambo ya kusaga vyakula mbalimbali vya kusaidia wajasiriamali wadogo na teknolojia za ufugaji samaki.

HABARI MICHEZO

# PARIMATCH YAMWAGA NEEMA MASHUJAA FC, YAANZA TAMBO

Na Mwandishi Wetu

ZIKIWA zimesalia siku chache kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kampuni ya michezo ya kubashiri ya Parimatch imetangaza rasmi kuingia makubaliano ya kuidhamini Mashujaa FC, imefahamika.

**Mashujaa FC ambayo imepanda daraja msimu huu itafungua pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24 kwa kuikaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.**

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa Parimatch Tanzania, Erick Gerald, wakati wa zoezi la utiaji saini wa mkataba ambalo lilifanyika kwenye ukumbi wa ofisi za klabu ya Mashujaa zilizopo jijini Dar es Salaam jana na kuhusisha viongozi wa pande hizo mbili.

Akizungumza jijini jana, Gerald alisema lengo la kuingia mkataba na klabu hiyo ni kukuza soko la mpira nchini pamoja na kuimarisha ushirikiano baina ya pande zote mbili.

"Parimatch tumekuwa wadau wakubwa katika sekta ya michezo hapa nchini na nje ya nchi, na kupitia udhamini huu unalenga kusaidia timu ambayo ina vijana wanaopata ajira, wanajenga afya na kuleta ushindani kwenye michezo," alisema Gerald.

Naye mwakilishi wa Mashujaa FC, Benjamin Kisinda, aliishukuru Parimatch Tanzania kwa kuwaamini na kuwaunga mkono.

Kisinda alisema udhamini ambao walioupata utawasaidia kupunguza changamoto za uendeshaji wa klabu yao.

Alisema timu yao inaendelea vyema na maandalizi na wamejipanga kuonyesha ushindani katika kila mechi ya Ligi Kuu Bara watakayocheza.

"Tunawashukuru wadhamini wetu Parimatch kwa kuja kuungana nasi katika kuendeleza soka, Mashujaa ni timu ambayo imepanda daraja msimu huu, kwa hivyo tunawakaribisha sana Kigoma katika familia ya Mashujaa," aalisema Kisinda.

Kampuni ya Parimatch imekuwa ikijihusisha na kubashiri michezo mtandaoni na imekuwa ikitoa ofa kubwa ya bonasi ya ukaribisho ya 125% hadi kufikia Sh.milioni moja kwa wateja wapya wanaojiunga nao.

Parimatch imekuwa ikifanya kazi Tanzania tangu mwaka 2019, hutoa mamia ya matukio kila siku kwenye michezo mbalimbali ikiwamo tenisi, mpira wa kikapu, kriketi na baseball.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Parimatch Tanzania, Erick Gerald (kushoto), akiwa na kiongozi wa Mashujaa FC, Benjamin Kisinda, wakisaini mkataba wa udhamini wa klabu hiyo jijini Dar es Salaam jana. Timu hiyo inajiandaa kushiriki Ligi Kuu Bara kwa mara ya kwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Beki wa Yanga SC asajiliwa Ihefu

Na Adam Fungamwango

WAKATI Ihefu imefanikiwa kumsajili mchezaji wa zamani wa Yanga, Paul Goedfrey 'Boxer' kwa kumpa mkataba wa miaka miwili akitokea Singida Fountain Gate, Kocha Mkuu wa timu hiyo, John Simkoko, amesema kikosi chake kiko tayari kwa vita ya kuwania taji la Ligi Kuu Bara.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana inasema mbali na beki huyo wa kulia, Ihefu pia imemsajili, Moubarack Amza kutoka Coastal Union FC, Ezekia Mwashilindi na Ismail Mgunda, wote wakitokea Prisons, Godfrey Manyasi aliyekuwa akikipiga Geita Gold.

Pia imefankiwa kuwabakisha kwa kuwaongezea mikataba wachezaji wake Never Tegere, Rafael Daudi, Lenny Kisu, Juma Nyosso, Fikirini Bakari, Rashid Juma na Hussein Masalanga.

Simkoko amesema timu yake imeimarika na iko tayari kuanza msimu mpya hata kama pazia lingefunguliwa leo.

"Kwa sababu imebaki wiki moja tutaitumia kujiandaa kimbinu zaidi dhidi ya wapinzani wetu Geita Gold, angalau tupambane kusaka ushindi katika mechi ya kwanza. Ni lazima tuwe na nidhamu ya mchezo, zimebaki siku saba na hizi tutatumia kukamilisha mikakati yetu ya kiufundi ili timu yetu katika michezo miwili tupate ushindi yote, au hata mechi ya ufunguzi," alisema.

Msimu uliopita wenyeji hao wa Mbarali walikuwa na msimu mzuri tofauti na walivyokuwa misimu mitatu nyuma.

## Coastal Union yatangaza hatari CCM Mkwakwani

Na Saada Akida, TANGA

KIKOSI cha Coastal Union kimetamba hakuna timu itakayovuna pointi kutoka katika timu hiyo kutokana na maandalizi bora waliyofanya kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka 2023/2024.

Pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara litafunguliwa Agosti 15, mwaka huu na Coastal Union watakuwa ugenini dhidi ya Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Kocha Mkuu wa Coastal Union, Mwinyi Zahera, alisema kikosi chake kimeimarika na tayari wachezaji wake wameonyesha wamejengeka kutokana na kiwango walichokionyesha walipoibuka na ushindi wa bao 1-0 katika mechi ya kirafiki dhidi ya Singida Fountain Gate.

"Tumejipanga vizuri, ligi itakuwa ngumu kwa sababu sasa hivi ukiangalia timu nyingi zimefanya usajili mzuri, kwangu tunataka matokeo mazuri katika kila mechi ya ligi. Nina wachezaji vijana ambao wataleta kitu na kufikia malengo," alisema Zahera.

Coastal Union jana ilitumia zaidi ya saa nne kufanya mazoezi kwenye Uwanja wa Popat Lal uliopo jijini hapa kutokana na uwanja wa Mkwakwani kutumika katika michuano ya Ngao ya Jamii.

## Gofu Morogoro mambo yaiva

Na Shufaa Lyimo

MASHINDANO ya wazi ya mchezo wa gofu mkoa wa Morogoro (Morogoro Open), yanatarajiwa kufanyika kesho mkoani humo, imefahamika.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Ofisa Habari wa Klabu ya Gofu ya Lugalo, Meja Selemani Semunyu, alisema maandalizi kuelekea michuano hiyo yanaendelea vyema.

"Tunaomba klabu zote zijitokeze kwa wingi kushiriki katika mashindano haya ambayo yanatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa, tunaamini kila klabu imejipanga vyema," alisema Semunyu.

Aliongeza kwa upande wa wachezaji kutoka Lugalo wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanaiwakilisha vyema klabu yao na kuendelea kuvuna makombe mbalimbali.

"Tunaamini hakuna kitu kitakachoharibika kwa sababu wachezaji wetu wanaendelea kujinoa kila siku, kila mmoja anataka kuona wanapata matokeo bora," aliongeza kiongozi huyo.

## ZISIKUPITE

### BAYERN YAMKOMALIA KANE

KLABU ya Bayern Munich wanataka kuwasilisha ofa mpya ya euro milioni 110 kwa ajili ya mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 30. ***(Sky Sports)***

### ORBAN KUMRITHI KANE

IWAPO Harry Kane ataondoka Tottenham Hotspur, klabu hiyo itafuatilia kumnunua mshambuliaji wa Gent, ambaye ni raia wa Nigeria, Gift Orban, mwenye umri wa miaka 21 pamoja na beki mwingine wa kati na kiungo. ***(Times)***

### ARSENAL, HOTSPUR VITANI

ARSENAL na Tottenham Hotspur zipo katika mbio moja ya kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Aston Villa Mbrazil Douglas Luiz, 25. ***(Football Insider)***

### RAYA SAFI ARSENAL

KLABU ya Arsenal imefikia makubaliano na Brentford ya kumsajili kipa wa Hispania, David Raya, mwenye umri wa miaka 27, kwa dau linalokaribia pauni milioni 30. ***(Fabrizio Romano)***

### NEYMAR ANUKIA SAUDIA

KLABU ya Saudi Arabia, Al-Hilal inataka kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Brazil, Neymar na inapanga kukutana na baba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31. ***(Footmercato)***

### NEYMAR ATAJWA BARCELONA

NEYMAR atakuwa tayari kuondoka PSG na kujiunga na klabu moja nchini Saudi Arabia ikiwa watamruhusu akae kwa mkopo Barcelona kwa msimu mmoja. ***(Sport)***

### MAGUIRE ANUKIA EVERTON

EVERTON inafikiria kumnunua mlinzi wa England, Harry Maguire, 30, huku Manchester United ikimtaka kiungo wa kati wa Ubelgiji, Amadou Onana, mwenye umri wa miaka 21. ***(Mirror)***

### TODIBO AKARIBIA UNITED

KLABU ya Manchester United inavutiwa na beki wa kati wa Ufaransa, Jean-Clair Todibo, 23, kutoka Nice ambaye kama mbadala wa Harry Maguire. ***(RMCSport)***

### BISSAKA KUULA UNITED

KLABU ya Manchester United inataka kuanza mazungumzo rasmi ya kumpa mkataba mpya na beki, Aaron Wan-Bissaka, 25. ***(Mail)***


### WALKER KUBAKIA CITY

MLINZI wa kulia wa England, Kyle Walker, 33, ameamua kubakia Manchester City, licha ya kufikia makubaliano ya awali ya kujiunga na Bayern Munich. ***(Athletic)***

### DARVICH NA BARCELONA

KLABU ya Barcelona imeongeza kipengele cha kutolewa cha euro bilioni moja kwenye mkataba wa kiungo wa kati wa Ujerumani, Noah Darvich, mwenye umri wa miaka 16. ***(Football transfers)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK AHITAJI UTULIVU LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

NAHODHA wa Liverpool, Virgil van Dijk, amesema anaelewa wasiwasi wa watu kuhusu klabu hiyo kushindwa kufanya usajili wa nguvu kabla ya msimu mpya na amewataka wachezaji wenzake kuongeza kasi baada ya kuondokewa na wachezaji kadhaa muhimu.

**Van Dijk mwenye umri wa miaka 32 alichukua nafasi ya Jordan Henderson kama nahodha baada ya kiungo huyo wa kati wa England kumaliza kuhudumu kwa miaka 12 Liverpool na kujiunga na klabu ya Saudi Pro League ya Al Ettifaq mwezi uliopita.**

Liverpool imepoteza wachezaji sita, huku Henderson na Fabinho wakihamia Saudi Arabia na viungo wenzake, Alex Oxlade-

**● ● ● Nahodha huyo asema wako tayari kwa changamoto mpya ingawa...**

Chamberlain, James Milner, Naby Keita na mshambuliaji, Roberto Firmino wakiondoka kwa uhamisho huru.

Ikiwa msimu mpya unaanza kesho, idadi ya waliowasili Anfield siyo ya kuridhisha, huku kiungo, Alexis Mac Allister na Dominik Szoboszlai wakiwa ndio wachezaji wawili pekee ambao Liverpool wamewasajili katika msimu huu.

"Ninaweza kuelewa kwa njia fulani," alisema Van Dijk alisema alipoulizwa kuhusu wasiwasi wa mashabiki wa Liverpool.

"Ni wazi, wakati wachezaji wengi wanaondoka, nahodha wako anapoondoka, makamu wako anaondoka, naweza kuelewa baadhi ya watu wana mashaka."

"Wacha tuangalie ikiwa wachezaji wengi wanaingia na tunapaswa kuwa tayari tena kwa msimu mrefu. Itakuwa ngumu sana tukiangalia timu zinazotuzunguka, lakini tunataka kuwa juu tena, tunataka kuwa na changamoto tena," alisema Van Dijk.

"Lazima tujiamini, tunapaswa kujiamini, na bado tunapaswa kujifunza kila siku.

"Kumekuwa na wahusika wanaoondoka, wachezaji ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio, lakini wengine wanapaswa kujitokeza. Hiyo ni changamoto nzuri kwa maoni yangu. Tunapaswa kufurahi."

Liverpool wataanza kampeni yao ya kuwania taji la Ligi Kuu England kwa safari ya kuwafuata Chelsea, mechi itakayochezwa Jumapili.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,142,1

MECHI KALI

SIMBA
VERSUS
SINGIDA BS FC

1 | 1.25
X | 4.85
2 | 8.25

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# CHELSEA YATAFUTA MBADALA WA NKUNKU

**LONDON,** England

CHELSEA itaamua iwapo itaongeza kasi ya kumsajili, Dusan Vlahovic baada ya mshambuliaji, Christopher Nkunku kuondolewa kwa "muda mrefu" kufuatia upasuaji wa goti, kwa mujibu wa ESPN.

Nkunku, aliyesajiliwa kwa euro milioni 60 majira ya joto kutoka RB Leipzig, alipata jeraha huko Chicago wakati wa mechi ya mwisho ya kirafiki, Chelsea ikiwakabili Borussia Dortmund wiki iliyopita.

Klabu hiyo ilisema katika taarifa Jumanne: "Nkunku amepata jeraha la goti ambalo litamfanya mshambuliaji huyo kukaa nje kwa muda mrefu.

"Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amefanyiwa upasuaji na sasa ataanza kujiuguza."

Dalili za awali zinaonyesha Nkunku anaweza kukaa nje ya uwanja kwa angalau miezi mitatu, habari ambazo zitakuja kama pigo kubwa kwa kocha mpya, Mauricio Pochettino.

Nkunku alikuwa mmoja wa wachezaji wa Chelsea waliofanya vizuri zaidi katika ziara yao nchini Marekani, akifunga mara tatu, huku Pochettino akijaribu kubadilisha kikosi kilichofunga mabao 38 pekee katika mechi 38 za Ligi Kuu England msimu uliopita.

Vyanzo viliiambia ESPN hitaji la klabu la kuwa na moto zaidi linaweza kuongeza nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa Juventus, Vlahovic, ambaye ni sehemu ya mazungumzo magumu yanayojumuisha kuondoka kwa Romelu Lukaku.



# David Raya huyoo Arsena

**LONDON,** England

ARSENAL imekubali ada ya karibu pauni milioni 30 kumsajili mlinda mlango wa Brentford, David Raya, vyanzo vimeiambia ESPN.

Maslahi binafsi yanakamilika na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 anatarajiwa kuwa mchezaji wa nne kusajiliwa na washikabunduki hao baada ya Declan Rice, Jurriën Timber na Kai Havertz.

Usajili wa Raya utachukua matumizi ya klabu hiyo msimu wa joto hadi zaidi ya pauni milioni 230 na atachukua nafasi ya mchezaji, Matt Turner, ambaye amejiunga na Nottingham Forest.

Nia ya klabu hiyo kwa Raya ilianza tangu mwaka 2020 na sasa Aaron Ramsdale ambaye ni kipa namba moja wa Arsenal yupo katika changam

Akijibu kuhusu uv
Raya anaweza kus
dana naye kwenye U
ja wa Emirates kwa n
ya kuanza, Ramsdale
iambia ITV Sport: "Fa
hivyo. Hakuna kitu k
chokuja kirahisi ka
soka.

"Ikitokea, itatokea
kisha tutapigana na
atengeneza kila m
toleo bora la sisi weny
kwa sababu ndivyo m

32,257/-

# KMC FC YAIWEKA YANGA MTEGONI UFUNGUZI BARA

**Na Saada Akida,** TANGA

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Abdihamid Moalini, amesema amedhishwa na utimamu wa mwili kwa wachezaji wake lakini anaendelea 'kuwasoma' wapinzani wao Yanga kuekelea mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 15, mwaka huu.

KMC itacheza mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya bingwa mtetezi, Yanga, Agosti 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

**Akizungumza na Nipashe jana, Moalini, alisema anatumia siku chache zilizosalia kwa ajili ya kutengeneza muunganiko wa wachezaji wake kabla ya kukutana na mabingwa hao watetezi katika mchezo huo wa kwanza.**

Moalini alisema kikosi chake kilifanya mazoezi mbalimbali ikiwamo ya utimamu wa mwili, mbinu za ufundi kwa muda wa wiki tatu, jambo ambalo limeimarisha wachezaji wake.

Kocha huyo alisema kazi kubwa aliyonayo sasa ni kuhakikisha nyota wake wanakuwa na muunganiko kwa sababu ya uwapo wa wachezaji wapya na zamani.

"Maendeleo ni mazuri, tumetumia vizuri wiki mbili za maandalizi ya msimu mpya, kwa ajili ya kujenga utimamu wa mwili, sasa bado nafanyia kazi muunganiko, naamini muda wa siku saba zilizobakia tutazitumia vizuri ili kupata matokeo chanya dhidi ya Yanga," alisema kocha huyo.

Wakati huo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa KMC, Daniel Mwakasungula, alisema baada ya kukamilisha usajili, timu yao iliweka kambi ya muda mrefu mkoani Morogoro.

"Sasa ninavyozungumza tayari kikosi kipo Dar es Salaam kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wao dhidi ya Yanga. Kocha Moalini bado ni mgeni lakini tumempa muda kidogo wa kutengeneza timu yake," alisema ofisa huyo.




Wachezaji wa KMC inayoshiriki Ligi Kuu Bara wakifanya mazoezi ili kujiandaa na mechi ya kirafiki dhidi ya KMKM itakayochezwa leo visiwani Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dodoma Jiji yatema cheche



**Na Abdallah Mataka**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi ya kirafiki dhidi ya Geita Gold, mabosi wa Dodoma Jiji FC wametamba kikosi chao kimejipanga kutoa vipigo kwa kila timu watakayokutana nayo kwenye msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mabao ya Dodoma Jiji katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro yalifungwa na Idd Kipagwile na Raizin Hafidh huku lile la kufutia machozi la Geita Gold likipachikwa wavuni na George Sangija, mchezaji mpya aliyesajiliwa kutoka Mbeya City.

Msemaji wa Dodoma Jiji, Moses Mpunga (pichani), alisema kikosi chao kimeimarika na wanafuraha kuanza msimu mpya kwenye uwanja wa nyumbani.

"Tunawakaribisha Coastal Union kwenye Uwanja wa Jamhuri, wanaufahamu vyema na sikumbuki mara ya mwisho ni lini walipata matokeo, ushindi wao zaidi ni sare, niwaombe waje kwa tahadhari, kauli yetu ni ile ile, iwe mvua, iwe jua ushindi lazima," alisema Mpunga.

Aliongeza Dodoma Jiji ina matarajio ya kufanya makubwa katika msimu mpya na sasa wanakamilisha maandalizi yao wakiwa kambini Morogoro.

Dodoma Jiji inatarajia kucheza mechi nyingine ya kirafiki leo dhidi ya KMKM kutoka Zanzibar.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/08/23 | 13:00 | Daejeon Citizen FC vs FC Seoul | 2.75 | 3.20 | 2.27 |
| 02. 13/08/23 | 13:30 | Incheon United FC vs Daegu FC | 2.25 | 3.10 | 2.80 |
| 03. 13/08/23 | 14:00 | Naestved BK vs Kolding IF | 2.75 | 3.25 | 2.23 |
| 04. 13/08/23 | 15:15 | FC Baden vs FC Vaduz | 2.65 | 3.20 | 2.33 |
| 05. 13/08/23 | 16:00 | IK Sirius vs Kalmar FF | 2.25 | 3.15 | 2.80 |
| 06. 13/08/23 | 16:00 | Brentford FC vs Tottenham Hotspur | 2.70 | 3.45 | 2.37 |
| 07. 13/08/23 | 16:00 | FC Nantes vs Toulouse FC | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 08. 13/08/23 | 16:00 | Hobro IK vs Vendsyssel FF | 2.39 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 13/08/23 | 17:00 | Cercle Brugge vs KRC Genk | 2.80 | 3.50 | 2.28 |
| 10. 13/08/23 | 17:00 | Motherwell FC vs Hibernian FC | 2.55 | 3.25 | 2.65 |
| 11. 13/08/23 | 18:00 | Burgos CF vs SD Huesca | 2.27 | 3.05 | 3.20 |
| 12. 13/08/23 | 18:00 | FF Jaro vs HIFK Helsinki | 2.55 | 3.20 | 2.42 |
| 13. 13/08/23 | 18:30 | Halmstads BK vs IFK Norrkoping FK | 2.55 | 3.10 | 2.46 |
| 14. 13/08/23 | 18:30 | Chelsea FC vs Liverpool FC | 2.70 | 3.50 | 2.35 |
| 15. 13/08/23 | 19:15 | Erzurumspor FK vs Bandirmaspor | 2.45 | 3.30 | 2.43 |
| 16. 13/08/23 | 20:00 | Estrela Amadora vs Vitoria SC Guimaraes | 2.65 | 3.10 | 2.60 |
| 17. 13/08/23 | 20:30 | Albacete Balompie vs Espanyol Barcelona | 2.95 | 3.15 | 2.35 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 10/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 17:00 | 4710 | Tobol Kostanay vs Derry City | 1.83 | 3.55 | 3.95 |
| 18:00 | 2699 | Nasaf Qarshi vs Buxoro | 1.26 | 4.73 | 9.66 |
| 18:00 | 3021 | Navbahor Namangan vs Pakhtakor | 2.22 | 2.85 | 3.15 |
| 18:00 | 5202 | FC Struga Trim Lum vs Swift Hesperange | 2.75 | 3.15 | 2.50 |
| 18:30 | 1017 | Sepahan Esfahan vs Teraktor Sazi | 1.74 | 3.21 | 4.68 |
| 18:30 | 4993 | TPS Turku vs JJK Jyvaskyla | 1.20 | 5.85 | 9.48 |
| 19:00 | 1332 | Simba vs Singida BS FC | 1.25 | 4.85 | 8.25 |
| 19:00 | 1425 | Zalgiris vs BK Hacken | 3.35 | 3.45 | 2.04 |
| 19:00 | 1576 | Sabah vs Partizan | 4.80 | 3.75 | 1.65 |
| 19:00 | 2929 | Karabakh vs HJK Helsinki | 1.55 | 3.90 | 5.60 |
| 19:00 | 3264 | Bodo Glimt vs Pyunik Yerevan | 1.24 | 6.00 | 9.40 |
| 19:00 | 4523 | Silkeborg Kfum vs Vendsyssel FF | 5.10 | 4.29 | 1.49 |
| 20:00 | 1082 | Sheriff Tiraspol vs BATE Borisov | 1.57 | 3.86 | 5.41 |
| 20:00 | 1345 | Valmiera Fk/Bjss vs Partizani Tirana | 2.79 | 3.23 | 2.43 |
| 20:00 | 1864 | Slavia Prague vs SC Dnipro 1 | 1.42 | 4.51 | 6.42 |
| 20:00 | 1942 | Omonia Nicosia vs Midtjylland | 3.40 | 3.30 | 2.07 |
| 20:00 | 2837 | Legia Warszawa vs Austria Vienna | 1.78 | 3.65 | 4.12 |
| 20:00 | 2848 | Dila Gori vs Apoel Nicosia | 3.15 | 3.15 | 2.24 |
| 20:00 | 2923 | Viktoria Plzen vs Gzira United | 1.19 | 6.02 | 13.05 |
| 20:00 | 3084 | Neftchi Baku vs Besiktas | 4.29 | 3.79 | 1.72 |
| 20:00 | 3401 | Santa Coloma vs AZ Alkmaar | 11.05 | 7.23 | 1.17 |
| 20:00 | 3581 | Rosenborg vs Hearts | 2.20 | 3.44 | 2.99 |
| 20:00 | 3919 | Akhmat Grozny vs Baltika Kaliningrad | 2.09 | 3.46 | 3.01 |
| 20:00 | 4996 | Sepsi Osk vs Aktobe | 1.76 | 3.54 | 4.39 |
| 20:00 | 5527 | Angelholms vs Eskilsminne IF | 5.24 | 4.03 | 1.49 |
| 20:30 | 3056 | Farul Constanta vs Flora Tallinn | 1.38 | 4.49 | 7.59 |
| 20:30 | 5352 | Hamrun Spartans vs Ferencvaros TC | 5.41 | 3.86 | 1.57 |
| 20:30 | 5960 | Hapoel Beer Sheva vs Levski Sofia | 1.66 | 3.74 | 4.79 |
| 21:00 | 1335 | Twente vs FC Riga | 1.20 | 6.02 | 12.04 |
| 21:00 | 1415 | KP Polonia Warsaw vs Siarka Tarnobrzeg | 1.38 | 4.28 | 7.14 |
| 21:00 | 1565 | Brugge vs KA Akureyri | 1.03 | 10.98 | 59.91 |
| 21:00 | 1921 | Throttur Reykjavik W vs IBV Vestmannaeyjar W | 1.58 | 3.95 | 4.30 |
| 21:00 | 2692 | NK Celje vs Neman Grodno | 1.93 | 3.35 | 3.80 |
| 21:00 | 3485 | Adana Demirspor vs NK Osijek | 1.79 | 3.51 | 4.21 |
| 21:00 | 3911 | B36 Torshavn vs HNK Rijeka | 6.39 | 4.39 | 1.44 |
| 21:00 | 4359 | Fenerbahce vs Maribor | 1.24 | 5.56 | 10.77 |
| 21:00 | 4375 | FC Arouca vs Brann | 1.93 | 3.44 | 3.69 |
| 21:00 | 4817 | Lech Poznan vs Spartak Trnava | 1.45 | 4.20 | 6.60 |
| 21:15 | 1029 | Aris Salonica vs Dynamo Kiev | 3.30 | 3.25 | 2.13 |
| 21:30 | 2405 | Afturelding vs UMF Grindavik | 1.38 | 4.75 | 5.66 |
| 21:30 | 3604 | Hibernian vs FC Luzern | 2.76 | 3.36 | 2.39 |
| 21:45 | 3654 | KF Ballkani vs Lincoln FC | 1.23 | 5.78 | 10.96 |
| 22:00 | 1018 | Zrinjski Mostar vs Breidablik | 1.74 | 3.65 | 4.30 |
| 22:00 | 1491 | Hajduk Split vs PAOK | 2.25 | 3.09 | 3.19 |
| 22:00 | 3593 | Rapid Vienna vs Debreceni VSC | 1.55 | 4.12 | 5.23 |
| 22:00 | 4022 | Olympiakos vs Racing Genk | 1.84 | 3.44 | 4.09 |
| 22:15 | 3291 | Grotta W vs Fram | 1.53 | 4.19 | 4.80 |
| 22:15 | 3636 | Keflavik W vs FH Hafnarfjordur W | 3.26 | 3.57 | 1.95 |
| 22:15 | 5513 | Ellidi vs Reynir Sandgerdi | 4.10 | 4.00 | 1.59 |
| 23:00 | 1142 | CD Alianza Cotopaxi vs Imbabura Sporting Club | 2.52 | 3.26 | 2.52 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



Raya huyo Arsenal UKURASA 22



Wachezaji wa Yanga wakishangilia bao katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya michuano ya Ngao ya Jamii iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga jana huku kiungo mpya wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto' (kulia) akisikitika. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# YANGA YATINGA FAINALI KIBABE

**Na Faustine Feliciane,** TANGA

## ●●● Ni katika michuano ya Ngao ya Jamii, Aziz Ki, Mzize waongoza...

MABAO mawili ya dakika za jioni kutoka kwa Aziz Ki na Clement Mzize yalitosha kuipa Yanga ushindi katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya kwanza ya michuano ya Ngao ya Jamii iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM, Mkwakwani jijini hapa jana.

**Kwa ushindi huo Yanga imetinga fainali na sasa itasubiri kukutana na mshindi wa mechi ya hatua ya nusu fainali ya pili ambayo inawakutanisha Simba dhidi ya Singida Fountain Gate FC.**

Yanga ambao ni mabingwa watetezi wa taji hilo jana walianza mpira kwa kasi na walitengeneza nafasi dakika za 13 na 20 hata hivyo haikuzaa matunda na kujikuta timu hizo zikienda mapumziko bila kufungana.

Iliwachukua dakika 19 tu kuanza kufanya shambulizi la nguvu kupitia kwa Keneth Musonda aliyeuwahi mpira baada ya kipa wa Azam, Zuberi Foba, kuukosa lakini shuti lake liliokolewa na beki, Nathaniel Chilambo na kuzaa.

Hata hivyo Yanga ilipata pigo dakika ya saba ya mchezo kutokana na mchezaji wake Makudubela 'Skudu' kuumia na kutolewa nje na nafasi yake kuchukuliwa na Crispin Ngushi.

Huku ikionekana kama timu hizo zitaingia kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti, Aziz Ki aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Farid Mussa aliwainua mashabiki wa Yanga kwa kufunga goli zuri dakika ya 85 baada ya kuwapiga chenga mabeki wa Azam na kupiga shuti lililomshinda Foba kudaka na kutinga wavuni moja kwa moja.

Dakika nne baadaye Mzize aliwahakikishia Yanga ushindi kwa shuti kali akiwa ndani ya eneo la hatari kwa kufunga goli la pili na kuamsha shangwe kwa mashabiki wa timu hiyo ambao walikuwa wakiisubiri hali hiyo kwa hamu.

Katika mchezo huo, Yanga walifanikiwa kuwakamata Azam katika maeneo yote na kutengeneza zaidi nafasi za kufunga ingawa washambuliaji wake wakiongozwa na Musonda na Max Nzingeli walishndwa kuzitumia vizuri nafasi hizo.

Kocha wa Yanga ni kama vile alitumia kipindi cha kwanza kuwasoma zaidi Azam na kuonyesha mabadiliko katika zaidi kipindi cha pili na kwa kumiliki mpira na kutengeneza nafasi nyingi na kufanikiwa kupata mabao mawili yaliyowapeleka hatua ya fainali.

Hata hivyo, mabeki wa Azam walijitahiji kutimiza majukumu yao kwa kuokoa hatari mara kadhaa dakika 45 za kwanza kutoka na kipa Foba kufanya makosa yaliyokuwa yakijirudiarudia.

Michuano hiyo itaendelea tena leo kwa Simba kuwakaribisha Singida Fountain Gate, mechi itakayochezwa kuanzia saa 1:00 usiku. Azam FC itakutana na timu itakayopoteza mechi ya leo katika mchezo wa kuwania mshindi wa tatu.

Yanga ilitwaa Ngao ya Jamii msimu uliopita kwa kuwafunga watani zao, Simba mabao 2-0, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Simba, Singida FG historia kuandikwa

**Na Saada Akida,** TANGA

WEKUNDU wa Msimbazi wanatarajia kuanza rasmi safari ya kuwania taji la kwanza msimu huu kwa kuwavaa Singida Fountain Gate FC katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya kuwania Ngao ya Jamii itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini hapa.

Mechi hiyo itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku na mshindi atatinga fainali ya michuano hiyo itakayofanyika Jumapili kwenye uwanja huo huo.

Akizungumza jana, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', alisema wachezaji wake wako tayari na mchezo huo na wamejipanga kufanya vizuri ili kutimiza malengo yao.

Robertinho alisema anahitaji kuona wachezaji wake wanajituma na kutinga fainali huku akiamini mchanganyiko wa wachezaji wapya na wale wa msimu uliopita utawasaidia kupata matokeo chanya.

Kocha huyo alisema anataka kufikia malengo kwa kutwaa Ngao ya Jamii na baadaye kulichukua pia taji la Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu haya mashindano lazima mmoja afunge, tunahitaji kutwaa Ngao ya Jamii, kufikia malengo hayo lazima tupambane kupata matokeo mazuri dhidi ya Singida Fountain Gate, baadaye fainali," alisema Robertinho.

Aliongeza anaimani kubwa na wachezaji wake watapambana ili kupata matokeo mazuri ambayo yanatarajiwa na mashabiki wa timu hiyo ambayo wanahitaji kupata furaha.

"Maingizo mapya yatakuwa machache, mashabiki wao wanatahutaji kuona timu yao inafanya vizuri kwa kushinda, kila mmoja wetu anahitaji matokeo mazuri yatakayotupeleka fainali na hatimaye kutwaa taji hili," Robertinho alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Singida Fountain Gate, Mathias Lule, alisema wanaiheshimu Simba lakini watapambana kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo.

"Simba ni timu kubwa, pia wamefanya usajili mzuri, lakini hata sisi tupo vizuri katika nafasi zote, naamini hatutaingia kinyonge kwa sababu tunawachezaji wazuri na wa kujivunia," alisema Lule.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >